Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

**Kikao cha Saba - Tarehe 9 Februari, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mheshimiwa Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:**

Taarifa ya Hesabu zilikaguliwa za Mfuko wa Bima ya Afya kwa Mwaka Ulioishia tarehe 30 Juni, 2003 *(The Report of Audited Accounts of the National Health Insurance Fund for the the year ended 30th June, 2003).*

## MASWALI NA MAJIBU

**Na. 70**

**Gari la Kituo cha Afya Mlalo**

**MHE. CHARLES H. KAGONJI** aliuliza:-

Kwa kuwa mara kwa mara Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais akiwa Mlalo aliahidi kuwa gari la kuhudumia kituo cha Afya Mlalo lingepatikana si kwa muda mrefu lakini hadi sasa gari hilo halijapatikana:-

(a) Je, kwa nini gari hilo halijapatikana hadi leo?

(b) Je, ni kawaida Serikali kukaa na ahadi zake yenyewe hata baada ya kuzirudia mara kwa mara kwa wananchi wenyewe?

(c) Je, ni lini sasa Serikali inatuahidi kutupatia gari hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali Mheshimiwa Charles Kagonji, Mbunge wa Mlalo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ninafahamu juu ya tatizo la kutokuwepo kwa gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Mlalo na uhaba huu uko katika Vituo vingi vya Afya hapa nchini. Serikali ina nia nzuri ya kuhakikisha kuwa kila Kituo cha Afya hapa nchini kinapatiwa gari la wagonjwa. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa Bajeti Serikali imekuwa ikinunua magari ya Vituo vya Afya kidogo kidogo kupitia Bajeti za Halmashauri kulingana na vipaumbele vya Halmashauri husika na upatikanaji wa fedha. Hivyo, ahadi ya Serikali ya kukipatia Kituo cha Afya cha Mlalo haijatekelezwa kutokana na ufinyu wa Bajeti. Hata hivyo, bado ninaendelea kuishauri Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kulipatia kipaumbele suala hili katika Bajeti yake hususan ya mwaka 2005/2006.

(b) Mheshimiwa Spika, si kawaida kwa Serikali kukaa na ahadi zake yenyewe. Nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa inaboresha huduma za jamii na kutekeleza ahadi ilizojiwekea. Hata hivyo, kama nilivyotangulia kusema utekelezaji wa ahadi hizo kwa sehemu kubwa unategemea zaidi upatikanaji wa fedha. Hadi sasa Serikali imeshanunua magari ya Vituo vya Afya vya Mnazi na Mlola.

(c) Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya 2004/2005 Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ilitenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa gari la Kituo cha Afya cha Mlalo, lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti ununuzi haukufanyika. Ununuzi huo sasa unategemea kupangwa katika mwaka wa fedha wa 2005/2006.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza, kwa sababu Vituo vya Afya kama hiki cha Mlalo kina watu wengi, kuna Vijiji nane, *Secondary Schools* mbili na tunafungua nyingine. Pia kuna Taasisi kadhaa, Mahakama na Polisi. Pamoja na ufinyu huo wa Bajeti unaosemwa, lakini kwa sababu ya kujali Afya za watu:-

(1) Je, Serikali haioni kwamba ni vizuri ikaweka kipaumbele katika maeneo kama haya ili kuwaokoa wananchi kutokana na matatizo mengi ya magonjwa yanayojitokeza?

(2) Je, Serikali inao mpango wowote wa muda mrefu au muda mfupi ambao unaandaa taratibu za kuimarisha Vituo vya Afya hapa nchini, maana huko ndipo watu wengi wanapoishi; Je, upo mpango wowote wa namna hiyo ukianzia Mlalo kwenye Jimbo langu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nisema tu kwamba kwa upande wa Jimbo hili la Mlalo, wenzetu kidogo wana bahati angalau Vituo viwili tayari vina magari

mawili. Lakini najua Majimbo mengi tu ambayo kwa kweli hata gari moja kwenye Vituo vyao vya Afya bado hayajapatikana.

Lakini kubwa hapa ni kwamba nia ya Serikali ni kama anavyoieleza Mheshimiwa Charles Kagonji, Vituo vyote vya Afya na hasa vile ambavyo vipo umbali zaidi kutoka kwenye maeneo ya karibu na Hospitali katika hali ya kawaida vinastahili kupata kipaumbele kutokana na sababu ambazo zimeelezwa. Lakini naomba nisisitize tu kwamba nia ya Serikali iko pale pale na katika Bajeti mbili mfululizo tumekuwa tukiwasilisha maombi haya Serikalini kwa lengo la kupata magari kwa ajili ya Vituo vya Afya. Kwa hiyo tunalijua na ni sehemu ya kipaumbele isipokuwa tuna tatizo tu na jambo hilo la fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tunao mpango ambao wote mnaujua wa *Basket Funding* ambao lengo lake ni kuimarisha afya kwa ujumla kwenye Wilaya, Mikoa, Zahanati na Vituo vya Afya. Katika *component* hiyo, yapo mambo mengi ambayo yanafanyika ikiwa ni pamoja na ukarabati, matengenezo na upatikanaji wa vifaa. Kwa hiyo mpango upo isipokuwa unaweza usiwe *exhaustive* kwa sababu inabidi kwenda hatua kwa hatua hadi tutakapolimaliza tatizo hili.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza swali lifuatalo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali na Halmashauri ya Wilaya ya Singida imefanya kazi nzuri ya kununua magari haya kwa ajili ya Vituo vya Afya kadhaa kwa Wilaya nzima au kwa Vituo vilivyo katika Wilaya ya Singida Kaskazini na Singida Kusini, lakini kwa kuwa magari hayo sasa yameondolewa kwenye Vituo na yamepelekwa kwenye Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya kwa kazi nyinginezo ambazo sio zilizokusudiwa; Je, Serikali iko tayari kutoa maagizo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida ayapeleke magari yale kwenye Vituo vya Afya alivyokusudiwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima kubwa sana nimwambie Mheshimiwa Mohamed Missanga kwamba jambo hili litakuwa limeamuliwa na Halmashauri yako kwa kushirikisha Baraza zima la Madiwani. Kwa hiyo kwa kweli kama mnataka jambo hilo lirekebishwe, dawa ni kurudi pale pale kwenye Halmashauri na kutoa uamuzi ambao utawezesha magari haya kurudi kwenye Vituo vya Afya.

Lakini kwa upande wa Jimbo la Mlalo kwa mfano, Waziri alilazimika kutoa agizo la kupeleka magari haya kwenye Vituo vya Afya kwa kuwa na wao walifanya jambo kama hilo. Kwa hiyo kwa kutumia msingi huo tutahakikisha kwa kupitia Ofisi yetu kwamba tunapeleka maelekezo yatakayowezesha jambo hilo kufikiriwa upya kwa ajili ya kusadia jamii katika eneo lake.

**Na. 71**

**Vijiji Kuwa Miji Midogo.**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Wilaya ya Njombe kuna zaidi ya Vijiji kumi ambavyo vinategemewa kuwa Miji midogo kama ilivyo Miji midogo ya Makambako baada ya miaka kumi ijayo ikiwemo Miji ya Ilembula, Uwemba, Mtwango, Luduga, Mkogo, Lupembe nakadhalika:-

(a) Iwapo Vijiji au Miji hiyo itakuwa Miji midogo yenye Serikali zake za Miji; Je, uhusiano kati yao na Halmashauri ya Wilaya utakuwaje?

(b) Badala ya kuunda Serikali za Miji mingi ndani ya Wilaya moja; Je, kwa nini Wizara isiamue kupanga Vijiji vyote nchini katika ngazi kadhaa ili Vijiji viendeshwe kwa kuzingatia tofauti za kimazingira kwa sababu Vijiji vyote vitakuwa na wakazi wengi kama Miji ya sasa?

(c) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka makazi ya watu nchini, chini ya Wizara moja ili kudhibiti ukuaji holela wa Miji na Vijiji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifutavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Halmashauri huomba kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa Kijiji ambacho kimeendelezwa au kukua kimji kuwa Miji Midogo. Kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa na Sera ya Maendeleo ya Makazi na kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Mipangomiji sura 378 ya mwaka 1956; basi Kijiji hicho hupewa hadhi ya kuwa Mji Mdogo.

Mji Mdogo ni Mamlaka kamili ya Serikali za Mitaa ingawaje huendelea kulelewa na Halmashauri ya Wilaya iliyoanzishwa. Kwa mfano Wajumbe watatu wa Mamlaka ya Mji mdogo kuchaguliwa kutoka miongoni mwa Madiwani wa Halmashauri husika. Halmashauri inaweza kuupatia Mji mdogo ruzuku ya fedha. Tunasisitiza kuwa ushirikiano wao si wa mkubwa na mdogo bali ni ushirikiano katika kuwahudumia wananchi.

(b) Mheshimiwa Spika, eneo lolote ili liweze kupata hadhi ya Miji masharti kadhaa lazima yazingatiwe yakiwemo haya yafuatayo:-

(i) Eneo hilo liwe limejengwa na kuendelezwa.

(ii) Liwe limetangazwa kuwa ni eneo litakalopangwa na kupimwa kwa kufuata taratibu za Mipangomiji, upimaji na pia kuwa chini ya Sheria ya Ardhi. Kwa hivi sasa ni Sheria ya Ardhi Na.4 ya 1999.

(iii) Liwe na idadi ya watu waliotajwa kwenye sera ya maendeleo ya makazi.

(iv) Liwe na uwezo wa kujiendesha kutokana na mapato yanayokusanywa kwa wananchi wake.

(v) Liwe na shughuli maalum ya utoaji huduma. Mfano kama ni Mji wa Makao Makuu ya Utawala au sehemu maarufu ya biashara au ni Kituo cha reli au usafiri wa anga na kadhalika. Kwa maana hii, tunachoeleza hapa ni kuwa haitakuwa rahisi Vijiji vyote nchini kuwa Miji na pale Kijiji kitakapofikia hatua ya juu zaidi kitapewa hadhi ya mamlaka ya Mji mdogo ambao ni kama Kijiji/Mji chini ya Sheria Na. 7 ya mwaka 1982. Tunachoweza kufanya sasa ili kuwa na mipango mizuri ya ujenzi katika Vijiji ni kutayarisha mipango ya matumizi ya Ardhi ya Vijiji (*Village Landuse Plan*). Katika Mipango ya matumizi ya Ardhi ya Vijiji, inawekwa bayana ardhi kwa ajili ya makazi, kilimo, majengo ya kuduma za umma na mapumziko, hata sehemu za upanuzi wa Kijiji wa baadaye hata hifadhi na kadhalika. Mipango hiyo ndiyo itakayoeleza kila Kijiji kuendelezwa kwa kuzingatia mazingira yake.

(c) Ni kweli kuwa kwa nchi nyingi zenye kufuata Utawala uliorithiwa kutoka Uingereza, masuala ya maendeleo ya Miji yameunganishwa na Maendeleo ya Makazi chini ya Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa. Jukumu la kupanga na kugawa majukumu wakati wa kuunda Wizara ni la mwenye mamlaka ya kuunda Wizara peke yake. Kwa misingi hiyo, utaratibu wa mgawanyo wa majukumu uliopo sasa ni mzuri na unafaa uendelezwe. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inahusika na uundaji wa mamlaka mbalimbali za Serikali za Mitaa na zaidi kuhakikisha kuwa sera za kisekta zinatekelezwa ipaswavyo na Halmashauri.

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi inahusika na utungaji wa sera zinazohusu Maendeleo ya Ardhi na Makazi na pia husimamia taaluma za wapima ramani, wathamini na Maafisa Ardhi katika maeneo mbalimbali na Maafisa Mipangomiji na kushughulikia masuala ya taaluma. Kwa mgawanyo huu wa majukumu, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa hakutakuwa na ukuaji holela wa Miji na Vijiji.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Katika kuuliza swali la msingi nimetoa mifano ya Miji/Vijiji zaidi ya kumi.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili ni kubwa kwa sababu hivi sasa si rahisi kwa Halmashauri za Wilaya kupeleka maombi kwenye Wizara husika ili iamue Kijiji fulani kiitwe Mji kama ilivyotokea kwa Mji mdogo wa Makambako. Tukiendelea na mwelekeo huu ni kwamba tunakabidhi Wizara nguo iliyochakaa na hivyo ikawa vigumu kushona. Je, si vizuri Serikali kwa kutambua madhara haya ikaanza kutengeneza sera ya kuoanisha Vijiji na Miji na kuwe na mratibu wa mara kwa mara ili tusichelewe kuamua Vijiji kadhaa kuwa Miji mapema na kuepuka matatizo ya Makambako?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jackson Makwetta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sera pamoja na Sheria zilizopo hivi sasa kwa kiasi kikubwa kabisa zinatosheleza kabisa kujibu tatizo tulilonalo. Tatizo ninaloliona mimi ni namna zinavyotekelezwa na Halmashauri zetu mbalimbali na ndio maana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa amelazimika kuchukua hatua zinazowezesha kuharakisha zoezi hilo kwa kutumia mamlaka aliyonayo kutangaza baadhi ya maeneo ambayo tunaona yako tayari kwa ajili ya kuwezeshwa kuwa katika nafasi ya Miji midogo akatangaza Miji 90 mara ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunaandaa uwezekano tena wa kutangaza Vijiji vingine ambavyo viko katika hatua hiyo, nadhani vinaweza vikazidi 100 ili tuweze kwenda na hili ambalo Mheshimiwa Jackson Makwetta analisema. Kwa hiyo, nadhani itategemea utekelezaji na usimamizi wa sera na Sheria zilizopo hivi sasa.

**Na. 72**

**Huduma ya Maji**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kata ya Itagano ya Mbeya Mjini na Kata ya Idini ya Mbeya Vijijini haziko katika mpango wa uboreshaji na usambazaji wa huduma ya maji katika awamu zote mbili ndani ya Manispaa ya Mbeya:-

(a) Je, ni lini wananchi wa maeneo haya watapata majisafi na salama?
(b) Je, ni lini wananchi hao watayaona matunda ya michango ya fedha walizoanza kuchanga?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji utakaotekelezwa kwa msaada wa Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika lake la Maendeleo *KFW* na Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(UE)* unatarajiwa kuanza mwezi Mei, 2005 baada ya kukamilika kwa zabuni ya kumtafuta Mkandarasi wa mradi huo. Aidha, Mradi utahusisha Kata zote za Manispaa ya Mbeya ikiwepo Kata ya Itagano. Hivyo basi, wananchi wa Kata ya Itagano watapata maji safi na salama mara baada ya mradi kukamilika.

(b) Mheshimiwa Spika, Kata ya Itagano hawatatoa mchango wa walengwa *(Local contribution)* kwani mchango huo umeshatolewa na utakamilishwa na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka - Mbeya.

Kata ya Ihango pamoja na Vijiji vyake vitano ambayo ipo nje ya mipaka ya Manispaa ya Mbeya, haihusiki na Mpango wa uboreshaji wa huduma ya maji katika Manispaa ya Mbeya.

Hata hivyo, mwaka 2000 wananchi wa Vijiji vya Idimi na Haporoto walibuni Mradi wa Majisafi utakaotumia teknolojia ya kutega *(gravity system)*. Wananchi hawa walichanga fedha ambazo zilitumika katika uchunguzi. Uchunguzi uliofanywa ulibaini kuwa Mradi wa kutumia teknolojia ya kutega maji utagharimu Shilingi milioni 95.4. Hivyo, upatikanaji wa majisafi na salama kwa wananchi hawa wa Kijiji cha Idimi na Haporoto utategemea juhudi na upatikanaji wa fedha za ujenzi wa mradi huo.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, napenda niipongeze Serikali kwa juhudi nzuri inazozifanya katika kuboresha suala zima la usambazaji wa maji ndani ya Mji wa Mbeya. Lakini katika michoro ya wafadhili wa Serikali ya Ujerumani chini ya Shirika la *KFW* inaonyesha Kata ya Itagano iko nje ya mradi huu. Ningependa kuiuliza Serikali ni chanzo kipi kitakachotumika kwa ajili ya kuwapatia maji watu hawa wa Itagano kwa sababu barabara ndio inayowatenganisha na wenzao wa Ihango, isingekuwa vema maji haya yakasambazwa kwa watu wote na kwa sababu wote ni Watanzania?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, kama ifuatavyo:-

Inawezekana kabisa Mheshimiwa Mheshimiwa Benson Mpesya michoro aliyoiona ni ile michoro au *design* za kwanza. Lakini *design* hizi za miradi hii ambayo inahusisha pia Mji wa Iringa na wa Mwanza imekwenda hatua mbalimbali za *variation* au mabadiliko. Pili, upande wa pili wa miradi hii utatekelezwa na Mamlaka zenyewe. Kwa hiyo mradi unafikisha maji sehemu ambayo iko karibu halafu Mamlaka zenyewe kwa sababu hazijitoi katika kutekeleza miradi na bado zinaendeleza miradi hadi iliyopo, kwa hiyo watafikisha sehemu ambazo ni ndogo, zinatumia *pipe* ambazo sio kubwa. Kwa hiyo napenda nimhakikishie kwamba mradi huu unahusisha Manispaa nzima ya Mbeya na utakwenda hatua kwa hatua. Lakini *component* kubwa itafanywa na *KFW* na wakati huo *supplementary project* zitafuata kwa kutumia fedha za Mamlaka.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mji wa Mbeya wanazungumzia Kata na Vijiji lakini Wilaya ya Geita haina maji mpaka sasa hivi na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ya Bajeti alisema kwamba Mji wa Geita utapata katika mwaka huu wa fedha na sasa hivi mwaka ndio unakatika:- Je, Serikali inasemaje kuhusu kuupa mji wa Geita maji kwa kipindi hiki cha mwaka wa fedha 2004/2005?

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, ingawa ni swali jipya lakini naona unayo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza sio kweli kwamba Mji wa Geita hauna miradi kama anavyosema. Kila mwaka fedha zimetengwa na zimepelekwa katika kuhudumia Mji huu ambao unakuwa kwa kasi. Ila muda wote tumekuwa tukitumia fedha zetu, sasa chini ya Mpango wa Maji Vijijini unaofadhiliwa kwa mkopo nafuu kutoka *World Bank*, Geita ni kati ya Wilaya ambazo ziko kwenye awamu itakayoanza mapema iwezekanavyo. Tunaelewa umuhimu wa Mji huu ambao unahudumia machimbo ya dhahabu ambayo yamezunguka Mji huu, kwa hiyo Serikali iko bega kwa bega katika kuhakikisha kwamba Mji wa Geita na wakazi wakishiriana na Mheshimiwa Mbunge wanapata majisafi na salama.

**Na. 73**

**Bandari ya Lindi**

**MHE. MARIA D. WATONDOHA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Bandari ya Lindi husafirisha mazao kutoka Wilaya za Ruangwa, Nachingwea, Lindi na Masasi kutokana na ukaribu wake kwa Wilaya hizo na kwa kuwa kina cha Bandari ya Lindi ni kifupi hivyo vyombo vinavyokuja ni vidogo hali inayosababisha malundikano wa bidhaa na kwa kuwa bidhaa nyingi muhimu hupitia Bandari ya Mtwara au barabara, hivyo kufanya bei za bidhaa hizo kuwa kubwa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta eneo mbadala lenye kina kirefu karibu na Lindi ili iwe Bandari inayokidhi mahitaji ya meli kubwa?

(b) Je, ni bidhaa kiasi gani zimepita katika Bandari ya Lindi kwa kipindi cha mwaka 2002/2003?

(c) Kama kuna bidhaa zimepita, zimeliingizia Taifa fedha kiasi gani na Shirika la Bandari kwa ujumla?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Watondoha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara inafuatilia kwa karibu sana utendaji kazi wa Bandari ya Lindi. Tarehe 03 Oktoba mwaka 2003 nilitembelea na kukagua Bandari ya Lindi na kushiriki katika Mkutano wa Wadau wa Bandari. Mkutano uliwashirikisha Viongozi wa Serikali katika ngazi zote, wafanyabiashara, wenye meli na Mamlaka ya Bandari Tanzania. Lengo la Mkutano lilikuwa kujadili changamoto zinazotukabili katika kuendeleza Bandari ya Lindi.

(b) Changamoto kubwa inatokana na kujaa kwa mchanga gatini licha ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa kuuondoa mchanga, Mradi ambao uliokamilika mwaka 1999 kwa gharama ya Shilingi takribani bilioni mbili. Ili kupata jawabu la muda mrefu,

Mamlaka ya Bandari kwa sasa inafanya utafiti wa kina wa namna ya kuondoa kabisa na kuzuia kulundikana kwa mchanga gatini Lindi.

Changamoto nyingine ni kushuka kwa bidhaa zinazozalishwa katika maeneo yanayohudumiwa na Bandari, ukaribu wa Lindi na Bandari kubwa ya Mtwara unafanya Lindi iwe na ushindani mkubwa. Matatizo yanayoikabili Bandari ya Lindi yakipatiwa ufumbuzi Bandari hii itakuwa na uwezo wa kuhudumia shehena na meli bila matatizo. Kwa sasa hakuna mpango mahsusi wa kutafuta eneo mbadala lenye kina kirefu kwa madhumuni ya kujenga Bandari.

(c) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003 jumla ya tani 9,800 za shehena zilihudumiwa na Bandari ya Lindi, shehena ambayo iliingizia Shirika la Bandari Shilingi milioni 27.1. Shehena iliyopakuliwa ni nafaka, sukari na saruji. Shehena iliyopakiwa ni mazao ya misitu, korosho, ufuta, karanga, mbaazi na chumvi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari inaahidi itafanya kila linalowezekana kuifufua Bandari hiyo. Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz na Waheshimiwa Wabunge wengine wa Mkoa wa Lindi ni watetezi wakubwa na waendelezaji wa Bandari kongwe ya Lindi, tunawashukuru. *(Makofi)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

(a) Kwa kuwa katika maelezo yake amesema tatizo kubwa la Bandari ya Lindi ni kujaa mchanga katika eneo la Bandari na kwa kuwa kihistoria Bandari ya Lindi ilikuwa na uvungu eneo la maji ambayo yanaruhusu kupita, lakini sasa Bandari wameziba, kwa hiyo inapokuja labda mvua mchanga unarundikana pale; Je, Serikali inalifahamu hilo na wataweza kulichukulia hatua mara moja?

(b) Kwa kuwa katika jibu lake Mheshimiwa Waziri ameonyesha kwamba bidhaa zinazopita pale zinashuka lakini si kwa sababu ya upungufu wa mazao; lakini kwa sababu tuna Bandari nyingine kubwa ya Lindi na kwa kuwa pale awali tulikuwa na MV. Lindi ambayo ilikuwa na *service* Bandari ya Lindi; Je, Serikali itaona uwezekano wa kututafutia *MV. Lindi* nyingine ambayo itaweza kutoa huduma ya uhakika kwa ajili ya Mji wa Lindi?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maria Watondoha, kama ifuatavyo:-

Kuhusu kuzibwa kwa matundu ya Gatini, ninakiri kwamba katika matengenezo ya Gati yaliyofanyika mwaka 1986 na baadaye mwaka 1999, kweli matundu ya Gati ya Lindi yalizibwa. Hilo ni tatizo mojawapo tulilolibaini linawezekana linaongeza tatizo

kubwa la kujaa kwa mchanga. Kwa hiyo, nakiri kwamba tumelibaini hilo. Lakini tatizo lingine vile vile tulilolibaini ni kwamba kuna mabadiliko makubwa ya mkondo wa mawimbi ya Bahari ambayo yanazidisha kulundikana kwa mchanga katika Bandari ya Lindi. Yote haya yataangaliwa katika usanifu unaofanywa na Mamlaka ya Bandari ili kuweza kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la pili ambalo ni Serikali kuangalia jinsi ya kuweza kupata meli nyingine kuhudumia Bandari ya Lindi badala ya *MV. Lindi.* Naomba tufanye kazi pamoja na Mheshimiwa Maria Watondoha na Wabunge wengine wa Mkoa wa Lindi ili kwa pamoja tuweze kuishawishi Sekta Binafsi iweze ikatusaidia katika kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la usafiri, si kwa ajili ya shehena tu, vile vile kwa ajili ya abiria kwa ajili ya Bandari ya Lindi. Kwa hiyo, tutashirikiana na Mheshimiwa Maria Watondoha.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, moja kati ya kero inayowasumbua watumiaji wa Bandari ya Lindi ni kwamba kwanza hakuna maboya ya kuongozea meli zile ndogo zinazoingia pale. Lakini pili hakuna taa za kuongozea meli hizo usiku zinapoingia mbali ya tatizo la mchanga, na tatu, kuna mmomonyoko mkubwa sasa unaoikumba Pwani ile kama Mheshimiwa Waziri alivyoiona mwezi Oktoba.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza sasa kuniangalia usoni na kuniambia Mkoa wa Lindi ni lini marekebisho haya yatatekelezwa ili wananchi waweze kutumia meli ile sasa?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, sina hakika kuhusu kumwangalia Mheshimiwa Bernard K. Membe usoni lakini naweza kuwaahidi wananchi wa Lindi kwamba yale yote aliyoyazungumza tutayatilia maanani katika usanifu tunaoufanya hivi sasa. *(Makofi)*

**Na. 74**

**Chombo cha Kusimamia Mazao Mchanganyiko**

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA** aliuliza:-

Kwa kuwa mazao mchanganyiko hayana chombo cha kuyaendeleza na kuyasimamia na kwa kuwa chombo kama hicho ni muhimu sana kuwepo:-

(a) Je, Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo kwa chombo cha aina hiyo?

(b) Je, chombo hicho kitaanzishwa lini kwa sababu ahadi ya Serikali imekuwa ni ya muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Daimon Mwaga, Mbunge wa Kibakwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kwamba mazao mchanganyiko hayana chombo maalum cha kuyasimamia kama ilivyofanyika kwa mazao mengine makuu ya biashara. Aidha, nimewahi kujibu mara kadhaa maswali mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge likiwemo Swali Na.318 la Mheshimiwa Job Y. Ndugai la tarehe 25/7/2003; Swali Na. 29 la Mheshimiwa Ally A. Karavina la tarehe 4/2/2004 na Swali Na.143 la Mheshimiwa Emmanuel E. Kipole la tarehe 18/2/2004 kuhusu rai ya kuwa na chombo maalum cha kusimamia mazao mchanganyiko.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetafakari suala hili na kuelekeza kwamba uamuzi wa kuunda chombo maalum cha kusimamia mazao mchanganyiko utafanyika baada ya kukamilika kwa Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo inayoandaliwa na Wizara yangu na kukamilika kwa taratibu zitakazowezesha Sera hiyo kuanza kutumika. Aidha, pamoja na kuweka Sera hiyo itakayoainisha aina na muundo wa chombo kinachohitajika na pia kuweka mwongozo wa namna ya kushughulikia hayo mazao mchanganyiko, Serikali itaangalia kwa kina gharama za uendeshaji wa chombo hicho kama zitakuwa na manufaa kwa wakulima hususan kwa kumwongezea zaidi mapato yatokanayo na mauzo ya mazao yake.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilieleza katika hotuba ya Bajeti ya Wizara yangu ya mwaka 2004/2005, maandalizi ya Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo yamefikia hatua za mwisho. Muda si mrefu itaweza kuwasilishwa Serikalini ili ipate kibali cha kutumika.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

(a) Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na jitihada zinazofanywa na Wizara, ningependa kufahamu kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, wakati wananchi wa Jimbo langu na Wilaya ya Mpwapwa wakisubiri chombo hicho kiundwe; kuna hatua gani za dharura au za muda mfupi za kuwawezesha wananchi hawa kuendeleza mazao yao ya alizeti, karanga na ufuta wakati wakisubiri chombo hicho kiundwe?

(b) Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri sasa atatoa ahadi gani ambayo ni ya uhakika kwa wakulima hawa wa karanga, alizeti na ufuta juu ya chombo hicho?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza tu nimpongeze Mheshimiwa Daimon Mwaga kwa jitihada anazozifanya katika kuhakikisha kwamba wananchi wa Jimbo lake wanapata ufumbuzi wa mauzo ya mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, hatua ambazo Serikali inazichukua katika suala hili la mazao mchanganyiko hususan haya ya mbegu za mafuta yanayolimwa katika eneo la Wilaya ya Mpwapwa, Kibakwe na Mkoa mzima wa Dodoma ni hili la kuhamasisha wakulima wetu mmoja mmoja na kupitia kwenye Vyama vyao vya Ushirika kuyasindika mazao haya ili yaweze kupata thamani zaidi na vile vile yaweze kuuzika kwa bei nzuri zaidi. Tumefanya warsha pale Dar es Salaam ya masoko ya ndani ambapo tuliitisha wafanyabiashara mbalimbali wakiwemo na watengenezaji wa hizi mashine ambazo zinaweza kusindika mazao yetu ambayo yanatumika hapa nchini. Kwa hiyo, hizo ni baadhi ya hatua ambazo sasa hivi Serikali inazichukua.

Mheshimiwa Spika, pili, katika suala hili la uundaji wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko, nimesema kwamba Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo itakapokuwa imekamilika itakuwa sasa ndio hatma ya kujua kwamba tunaweza kuanzisha lini kwa uhakika.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Katika juhudi za Serikali kuboresha masuala ya masoko ya mazao madogo kupitia Wizara hii limejengwa Soko la Kimataifa la mahindi Kibaigwa, Kongwa. Soko hili linauza zao moja tu la mahindi. Je, isingekuwa vizuri basi tukapata wataalam kutoka Wizara hii wakatusaidia kulibadili na kuliboresha soko hili ili likaweza kuuza pamoja na mahindi lakini pamoja na mazao mengine kama vile karanga, alizeti na mazao mengine madogo madogo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawashukuru sana wananchi wa Wilaya ya Kongwa kwa ushirikiano waliouonyesha katika kuhakikisha kwamba soko hili linajengwa kwa jitihada za wafadhili pamoja na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la wataalam wa kuweza kusaidia Soko hili ili liweze kuhusika na mazao mengine, pia nataka kusema kwamba pale lile soko lilipofikia sio mwisho kwa sababu shughuli nyingine bado zinaendelea kukamilika. Kusema kweli lile Soko tulisema liwe Soko la Nafaka na wataalam wetu wanaendelea kushirikiana na wananchi wa Wilaya ya Kongwa kuweza kuangalia uwezekano wa mazao mengine kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amependekeza.

**Na.75**

**Wanunuzi wa Pamba - Kilosa**

**MHE. CHRISTOPHER SEMANINI WEGGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Kilosa ni moja kati ya Wilaya zinazolima pamba, lakini pamba inayolimwa Kilosa ni bora zaidi kuliko pamba inayolimwa kwenye maeneo mengine nchini kwani pamba hiyo inatoa nyuzi ndefu na bora sana:-

Je, ni lini Serikali itapeleka wanunuzi wazuri Kilosa kununua pamba hiyo nzuri?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Christopher Semanini Wegga, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa linalosababisha kukosekana kwa wanunuzi wa pamba Wilayani Kilosa ni kiwango kidogo cha uzalishaji ambacho hakizidi tani 1,000 kwa mwaka. Kiasi hiki ni kidogo sana na hakiwashawishi wanunuzi kwenda kununua pamba hiyo kwa kuogopa kupata hasara kutokana na gharama kubwa za ununuzi. Pamoja na wanunuzi binafsi kutopendelea kwenda Wilayani Kilosa kununua pamba kutokana na uzalishaji mdogo, Serikali kupitia Bodi ya Pamba sambamba na juhudi za kuhamasisha kilimo cha pamba Wilayani humo, huwashawishi pia wanunuzi binafsi kwenda kununua pamba Kanda ya Mashariki inayohusisha pia Wilaya ya Kilosa. Pale inapotokea kuwa wanunuzi hao hawakujitokeza, Serikali huingilia kati na kuiruhusu Bodi ya Pamba kununua pamba katika eneo hilo moja kwa moja.

Juhudi za Serikali za kuwashawishi wanunuzi binafsi kwenda kununua pamba Kanda ya Mashariki imezaa matunda msimu wa ununuzi wa 2004/2005 ambapo Kampuni ya *Nyanza Cotton Oil* ambayo hununua pamba kwa wingi sana Kanda ya Magharibi imekubali kuja kununua pamba Wilaya za Ulanga, Kilosa, Mvomero na Morogoro. Aidha, Bodi ya Pamba itanunua pamba yote katika maeneo ambayo hayatafikiwa na wanunuzi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Wilaya ya Kilosa kukosa wanunuzi wa pamba linatarajiwa kupungua kwa kiasi kikubwa msimu wa mwaka 2005/2006 kufuatia Kampuni ya *New Msowero* kuamua kujenga kiwanda kipya cha kuchambua pamba katika Kijiji cha Msowero kilichoko Tarafa ya Magore. Kiwanda hiki kitakuwa na uwezo wa kuchambua tani 3,000 za pamba mbegu kwa mwaka. Changamoto iliyoko ni kwa wakulima na Wilaya ya Kilosa pamoja na maeneo yanayozunguka Wilaya hiyo kuongeza uzalishaji ili kukidhi mahitaji ya kiwanda hicho.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kukubali kwamba ni kweli kuna tatizo la ununuzi wa pamba Kilosa lakini akumbuke kwamba Serikali ilishatamka ndani ya Bunge hili hasa sauti nzito kama ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba atahakikisha pamba yote inanunuliwa na kwa bei nzuri ya Sh.290/= na yeye anakubali kwamba kuna tatizo la kilimo kidogo; unapotaka kuondoa umaskini utaanza na kuwahamasisha kununua hata hiyo ndogo ili umaskini utoke nao wahamasike kulima pamba nyingine. Sasa kuna mgongano Serikali inataka mpaka tulime pamba nyingi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Uliza swali.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Je, yuko tayari sasa kwenda kufidia pamba ile na kununua yote kwa bei ya Sh.290/= na huyo ambaye amewapunja sasa baada ya kuhangaika kutafuta Soko; Je, watamchukulia hatua gani? Ahsante Mheshimiwa. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri!

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Bado la pili.

**SPIKA:** Tumeshasikia.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** La pili bado.

**SPIKA:** Aaaaah, nimeshampa Mheshimiwa Naibu Waziri nafasi ya kujibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka niseme kwamba hapa hakuna migongano yoyote ambayo imejitokeza katika kauli. Kauli ya awali aliyosema kwamba ilitolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba pamba yote itanunuliwa na mimi kwenye jibu langu hapa ndivyo nilivyosema kwamba baada ya wanunuzi kukosekana, basi ilibidi Bodi ya Pamba moja kwa moja iende kununua pamba hiyo, hiyo ilikuwa ni kauli ya Mheshimiwa Waziri iliyokuwa imesemwa hapa. Kwa hiyo hapo hakuna mgongano wowote ambao umejitokeza.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu mapunjo ya bei, kwanza katika Kanda ile ya Mashariki ni tofauti kidogo na ile Kanda ya Magharibi ambapo kulikuwa na mkanganyiko wa bei iliyokuwa imetoka kwenye bei ya Dunia wakati ule na kusababisha kufanya marekebisho na kuweza kuwafanya wakulima wengine waweze kufidiwa. Kwa hiyo, kwa upande wa Kanda ya Mashariki, tatizo hilo la kwamba kuna kufidiwa bei au la, halipo.

**Na. 76**

**Kufuta Ushuru wa Forodha kwa Pembejeo za Kilimo**

**MHE. SAID JUMA NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Mkutano wa Bajeti wa 2004/2005, Serikali iliahidi kufuta ushuru wa forodha kwa pembejeo za kilimo na kuweka ruzuku ya usafirishaji kwa bidhaa hizo kwa lengo la kusaidia kupunguza gharama ya ununuzi kwa pembejeo hizo kwa wakulima:-

(a) Je, tamko hilo litatekelezwa vipi na limewanufaisha vipi wakulima?

(b) Kwa nini ruzuku ilitenganisha baadhi ya mbolea na kuzipa ruzuku tofauti kwa mfano Mfuko wa mbolea ya *Urea* na *DAP* ilipewa ruzuku ya asilimia 100 wakati

*CAN* ilipewa ruzuku chini ya asilimia 100 na *NPK* haikuhusishwa? Je, ni vigezo gani vilihusika kufanya mgawanyo huo wa ruzuku kwa pembejeo?

(c) Baada ya tamko hilo la Serikali, wafanyabiashara walipandisha kwa kiasi kikubwa bei ya mbolea; Je, lengo la Serikali lilikuwa kuwasaidia wafanyabiashara au wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba Serikali imefuta karibu kodi zote kwenye pembejeo na zana za kilimo na ni kweli pia kwamba katika mwaka wa 2003/2004 Serikali ilitoa ruzuku ya kufidia sehemu ya gharama za usafirishaji wa mbolea kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na kwa nchi nzima kwa mwaka wa 2004/2005. Uamuzi huu wa Serikali umetekelezwa kama ifuatavyo:-

- Wizara imewahimiza wafanyabiashara binafsi, Kampuni ya Mbolea ya Tanzania *(TFC)* na Kampuni ya Biashara ya Mkoa wa Dar es Salaam kuagiza mbolea kwa wingi na kuzisambaza Mikoani.

- Wizara imeteua Vituo 14 vya kusambaza mbolea ambavyo ni Iringa, Makambako, Songea, Mbeya, Sumbawanga, Bukoba, Mwanza, Tabora, Dodoma, Arusha, Dar es Salaam, Mtwara, Tanga na Morogoro.

- Mikoa na Wilaya zilitakiwa kuunda Kamati za kusimamia shughuli zote zinazohusiana na mbolea inayopewa ruzuku. Wizara iliigawia Mikoa mbolea kulingana na mahitaji yake na kusimamia upelekaji wa mbolea hiyo.

- Mikoa na Wilaya ziliteua mawakala wa kusambaza mbolea kwa wakulima na kupanga bei kwa Vituo mbalimbali ndani ya Wilaya, hususani Vijijini na kwenye Vituo vya biashara.

Hadi kufikia tarehe 04 Februari, 2005 tani 73,164.27 za mbolea mbalimbali za ruzuku zilikuwa zimefikishwa kwenye Vituo Vikuu vya Kusambazia Mbolea, zikiwemo tani 10,124.60 za mbolea ya *DAP* tani 29,445.65 za *UREA* tani 4,919.40 za *CAN*, tani 488.50 za *TSP* na tani 28,186.05 za *NPK*. Kati ya mbolea hizo, jumla ya tani 62,625.05 zimeuzwa.

Utaratibu huu umewezesha mbolea kuagizwa kutoka nje ya nchi na kusambazwa Mikoani kwa wingi zaidi kuliko ilivyowahi kutokea katika misimu iliyotangulia. Kwa mfano hadi tarehe 31 Mei, 2004 jumla ya tani 38,935 tu za mbolea mbalimbali za ruzuku zilikuwa zimefikishwa katika Vituo Vikuu vya Kusambazia Mbolea Mikoani.

Aidha, wakulima wamepata mbolea kwa bei nafuu kuliko ambavyo ingekuwa bila ruzuku na kwa utaratibu huu umefanya Kamati za Mikoa na Wilaya zisimamie usambazaji wa mbolea na hivyo kuzuia bei za mbolea kupandishwa kiholela.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba viwango tofauti vya ruzuku vimetolewa kwa aina tofauti za mbolea. Mbolea zenye virutubisho vingi kwa kilo zimepewa ruzuku kubwa kuliko zile zenye virutubisho kidogo ili kuwavutia wakulima wanunue aina za mbolea zenye virutubisho vingi. Aidha, mbolea zinazoharibu udongo au mazingira, kwa mfano, *sulphate of Ammonia* hazipewi ruzuku kabisa ili kuwashawishi wakulima waache au wapunguze kuzitumia.

(c) Habari tulizonazo ni kwamba mwanzo wa msimu wa kilimo na kabla mbolea za ruzuku hazijafika Mikoani, wafanyabiashara waliokuwa na mbolea waliziuza kwa bei kubwa lakini bei hizo zilishuka baada ya mbolea za ruzuku kufikishwa Mikoani. Lengo la Serikali linajulikana, nalo ni kuwafikishia wakulima mbolea kwa wingi na kwa bei nafuu kadri inavyowezekana.

**MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu kwamba ingawa nia ya Serikali ni nzuri lakini utekelezaji wa jambo hili umekuwa mgumu na kwamba mbolea hii anayosema tani 38,000 na yeye anaona ni nyingi anafahamu kwamba haya ni mahitaji ya Mkoa mmoja tu kama vile Ruvuma au Iringa na anajua sasa kwamba nchi nzima ina matatizo makubwa na upungufu wa mbolea? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, mimi nafahamu tatizo hilo sana tena kwa kina na mapana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini tusisahau humu humu Bungeni tumeshapata kusifiwa kwa jinsi tunavyojitahidi kukabiliana na matatizo haya kwa nchi hasa tukifikiria matatizo ya barabara, mvua na kadhalika. Mheshimiwa Makinda ni mmoja aliyetusifu kwa jitihada tulizofanya. Kwa hiyo, ninachotaka kusema, si kweli kabisa kwamba tumefanya kazi isiyopendeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili nataka kusema hivi, tani zilizouzwa mpaka sasa ni 62,000, zilizopelekwa Mikoani ni 73,164.24 lakini mpaka tarehe ya juzi juzi hapa mbolea zilizouzwa ni 62,665.05 na sio 38,000 anazosema Mheshimiwa Mbunge. Takwimu hizi nilizitoa mwenyewe hapa hapa Bungeni. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, pamoja na matatizo haya, tuzidi kushirikiana na Kamati za Mikoa kukabiliana na tatizo hili. Tunafanya kazi! *(Kicheko)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Serikali imejiingiza katika kutoa ruzuku kwa mbolea ambapo ni kitu kizuri na kwa kuwa hatutegemei kwamba baadaye itajitoa; Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba wakati umefika wa kufufua viwanda vya mbolea kwa vile sasa tunayo gesi

ya Songosongo ili viweze kufanya kazi zaidi kuliko kutegemea mbolea ya kununua na kutoa ruzuku?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli naungana naye kwamba upo umuhimu wa kushughulikia suala hili na linazungumzika lakini kwa vile linahitaji zaidi ya Sekta ya Kilimo maana yake viwanda, Wizara ya Fedha na kadhalika, sio rahisi kutoa jibu lakini azma hiyo ipo, tunataka kutoa huduma hii bila kulegalega.

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wa Manispaa ya Iringa wanashukuru sana kwa ruzuku hiyo iliyotolewa na Serikali lakini kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kwamba Mkataba wa ruzuku ulifanywa kwa baadhi tu ya wafanyabiashara wakubwa kama *TFC* na wafanyabiashara binafsi kama *STACO* na hivyo kusababisha wafanyabiashara hawa wakubwa kuishiwa mapema na hivyo kusababisha wale ambao hawakuingia katika Mkataba wa ruzuku hiyo kuuza kwa bei kubwa kama ilivyotokea katika Manispaa ya Iringa.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali itakubaliana nami kwamba ni vizuri Mkataba wa ruzuku ukafanywa kwa wafanyabiashara wote wanaohusika na pembejeo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, matangazo yalitolewa na kualika wafanyabiashara washiriki na kwa bahati mbaya waliojitokeza ni hawa na hao wengine hawakujitokeza.

Kwa hiyo, hatukuwa na namna ya kuwalazimisha wafanye hivyo. Lakini zaidi ya hapo, hiyo mbolea iliyopotea ni kwa muda tu mbolea nyingi zimeshaagizwa na zinaendelea kusambazwa, sio suala la kusimama na kungoja, hapana linaendelea. Tunachoomba tu Mheshimiwa Mbunge tuzidi kushirikiana na Kamati za Mikoa na Wilaya kufanikisha lengo hili. Ni azma yetu kusaidia wananchi wetu.

**Na. 77**

**Chombo Kinachosimamia Michezo Nchini**

**MHE. AZIZA S. ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa *FAT* ni chombo kinachosimamia michezo hapa nchini na kwa kuwa vipo Vilabu ambavyo vinashiriki michezo hiyo kama vile Yanga, Simba na kadhalika:-

Je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuviimarisha Vilabu hivyo ili viweze kufanya vizuri na michezo iweze kuimarika hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni vigumu Serikali kusimamia vilabu kama vile vya Simba na Yanga kwa sababu Serikali kwa ujumla ina wajibu wa kusimamia maendeleo ya michezo yote nchini. Pale unapohitajika msaada, Serikali inasaidia kufuatana na uwezo wake kwa wakati huo. Aidha, Mheshimiwa Spika, Vilabu vya Michezo vyote nchini vinapaswa kujisimamia vyenyewe bila ya msaada wa Serikali.

**MHE. AZIZA S. ALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vilabu vya Simba na Yanga vina wapenzi wengi hapa nchini na hata humu Bungeni tuko wengi na kwa kuwa ni Vilabu vyenye migogoro mingi sana ambayo inapunguza ari ya michezo katika nchi hii; Je, ni nini chanzo cha migogoro katika Vilabu hivyo?

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua hatua gani ili kuweza kusaidia kupunguza migogoro ambayo iko kwenye Vilabu hivi ili kurudisha ari ya wanamichezo au ya wapenzi kama ilivyokuwa ikifanya kwa vijana wetu wa *Serengeti Boys*?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kumekuwepo na migogoro ya mara kwa mara katika Vilabu hivi vya Simba na Yanga. Migogoro ambayo ni kweli imeshusha ari ya wapenzi wa soka na wengine hata kususa kwenda Uwanjani.

Chanzo kikubwa cha migogoro katika Vilabu hivi viwili ni ulaji. Watu pale hawagombei nafasi ili kuendeleza Mpira lakini wanagombea nafasi ili watumie mapato yanayoingizwa na Vilabu hivyo kula. Wapo watu pale hawana shughuli yoyote aidha, biashara au kazi, lakini wanaishi kwa kutegemea mapato ya Vilabu hivi.

Hatua za Serikali ni kwamba, pale tunapoona kwamba migogoro hii inataka kuhatarisha amani, Serikali huchukua hatua kadhaa. Tumeshiriki katika kutatua mgogoro wakati Simba, Kamati yote ya Utendaji ilipojiuzulu .Lakini vile vile tumejitahidi pamoja na ninyi Waheshimiwa Wabunge mmewaita hapa Yanga karibu mara mbili, Waziri Mapuri kawaita, lakini kuna wengine katika makundi hayo hawasikii la Mwadhini wala ya mchota maji Msikitini, lakini itakapofikia kuhatarisha amani Serikali itatumia nguvu zake. *(Kicheko)*

**MHE. SALOME J. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa mchezo wa Mpira wa Miguu ni maarufu sana nchini kwa wanawake na wanaume na kwa kuwa hivi karibuni timu ya *Serengeti Boys* iliibuka na kufanya vizuri sana kiasi cha kuingia fainali; Je, Serikali inaweza kuliambia Bunge hili ni nini hasa

kimetokea na nini sasa *position* ya timu hii baada ya kugundulika kwamba mchezaji mmoja alikuwa amezidi umri kiasi cha timu hii kunyimwa kuendelea mbele? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli *Serengeti Boys* walifanya vizuri sana lakini kilichotokea hadi kuondoshwa katika mashindano haya ni wenzetu wa *CUF* kutokuelewa usahihi wa mambo ulivyo. *CUF* sio hii ya Chama *CUF,* ile ya Shirika la Michezo la Mpira wa Miguu Afrika. Ukweli ni kwamba wao wanadai Nurdin Bakari amezaliwa mwaka 1983 na kigezo chao ni *Affidavit* ambayo ilipelekwa na Klabu yake ya Simba. Lakini *Serengeti Boys* ilipeleka *Original Birth Certificate* ambayo imesainiwa na Msajili wa Vizazi na Vifo mwaka 1994 hata mashindano haya ya *Age Category* hayajaanzishwa. Kwa hiyo, sisi tume-*appeal* kwao tukiwaambia kwamba mahali ambapo kuna hati yenyewe si vema wala si busara kung'ang'ania kutoa maamuzi kwa kutegemea *Affidavit*.

Mheshimiwa Spika, ndio tunasema hatua hiyo tuliyochukua ya kukata rufaa inatupa matumaini kwamba *Serengeti Boys* watarejeshwa katika mashindano haya.

**SPIKA:** Tuachane na *Serengeti Boys* tuendelee na maswali ya Wizara ya Elimu na Utamaduni. Mheshimiwa William Shellukindo, endelea na swali lako. *(Kicheko/Makofi)*

**Na. 78**

**Mpango Endelevu na Kuboresha Elimu ya Msingi**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) umeongeza hamasa kubwa kwa wananchi na kuzipa sura mpya Shule za Msingi nchini; kwa kuwa mpango huo unatekelezwa kwa msaada kutoka kwa Wahisani wa nje:-

(a) Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kuhakikisha kwamba moto iliyouwasha na kuziwekea mazingira mazuri na ya kudumu Shule za Msingi zilizopo na zile mpya kwamba hauzimiki?

(b) Kwa kuwa, Elimu na hasa ya Msingi ni haki ya msingi ya kila Mtanzania; Je, si vyema kutenga asilimia fulani katika bajeti nje ya *ceiling* ya bajeti ya kila mwaka ya Wizara ya Elimu na Utamaduni?

(c) Kwa kuwa, haki hiyo ya msingi ya kila Mtanzania inatekelezwa pia na asasi zisizo za Kiserikali, je, si vyema na asasi hizo nazo zikapewa msaada chini ya MMEM?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) 2002-2006 unakuwa endelevu Serikali inahakikisha mambo matatu yafuatayo:-

(i) Uchumi wa Taifa unaendelea kukua kwa zaidi ya mara mbili ya ongezeko la watu na mapato ya Serikali yanazidi kuongezeka ili kuipa Serikali uwezo wa kumudu gharama za huduma za jamii zinazozidi kuongezeka zikiwemo gharama za elimu kama vile za uendeshaji wa Shule, matengenezo ya majengo ya Shule na upanuaji wa Shule kutokana na bajeti ya Serikali.

(ii) Kuandaa na kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) 2004-2009 kwa lengo la kuongeza wahitimu wa Elimu ya Msingi wanaoendelea na Sekondari kutoka asilimia 20 ya kabla ya mwaka jana 2004 hadi 50 ifikapo mwaka 2009 ili kuwapa wazazi na wanafunzi wa Shule za Msingi matumaini ya kuendelea katika Elimu ya Sekondari.

(iii) Kuongeza ubora wa Elimu ya Msingi na Sekondari ili iwe na manufaa ya uhakika katika soko la ajira pamoja na kujiajiri na aidha kuweza kumudu masomo ya Elimu ya Sekondari na Elimu ya Juu pamoja na ushindani katika soko huria na dunia ya utandawazi.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Elimu ya Msingi ni haki ya msingi ya kila Mtanzania na ndiyo maana Serikali ikaandaa mpango maalum MMEM 2002-2006 wenye lengo la kuifikisha elimu hii kwa watoto wote wa rika la Elimu ya Msingi yaani wa miaka 7-13 ambao mwaka 2000 Bunge hili lilipochaguliwa walikuwa Shuleni asilimia 58 tu lakini mwaka jana walifikia asilimia 91 na mwaka huu tunategemea watafikia asilimia 95 au zaidi kidogo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa kutenga asilimia fulani nje ya *ceiling* ya bajeti ya Wizara yangu ili kuwa na uhakika wa kuendeleza mafanikio haya ya elimu unavutia sana na inafaa uzingatiwe na mafundi wa mambo ya bajeti ya Serikali.

Lakini kwa uhakika mwingine mimi nawaomba wananchi wawachague tena Waheshimiwa Wabunge wa sasa wenye uzoefu wa kupitisha bajeti kubwa ya elimu. *(Makofi)*

(c) Kwa sasa mpango wa Serikali kupitia MMEM 2002 hadi 2004 ni wa kutoa ruzuku ya maendeleo na ruzuku ya uendeshaji wa Shule za Msingi za Serikali peke

yake ambazo kwa Shule za Msingi za Serikali peke yake ambazo ndizo zinazotoa Elimu ya Msingi kwa karibu watoto wote. Watoto wanaosoma katika Shule za Msingi zisizo za Serikali sehemu kuwa wanasoma katika Shule za Msingi zinazotoa Elimu ya Msingi kwa lugha ya Kingereza na wazazi wanao uwezo wa kulipia na ndiyo maana wameamua wenyewe kupeleka watoto wao katika shule hizo.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na yenye matumaini, napenda tu kuungana na Mheshimiwa Waziri kwamba kuna haja kwa kweli kuwekea msingi mzuri wa Elimu ya Msingi ili iwe endelevu. Sasa kwa kuwa bajeti ya Wizara ya Elimu yenyewe haitoshelezi mahitaji yake na tukiweka *ceiling* katika bajeti hiyo haitasaidia.

Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba sasa kuna haja ya kuamua kwamba asilimia fulani kama asilimia 2 ya pato la Taifa litengwe kwa ajili ya elimu na hasa Elimu ya Msingi na kuanza kuwekwa kwenye Mfuko wa Elimu ulioanzishwa kwa sheria Na. 8 ya mwaka 2001 ili kujihakikishia uendelevu huo?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi, mimi navutiwa sana na wazo hili. Kwa hiyo ningependa kumshauri Mheshimiwa Shellukindo kwamba kwa kuwa yeye ni mzoefu sana wa mambo ya utawala na mambo ya Serikali, azidi kulijenga wazo hili katika Vikao vyetu vya Kamati za Bunge na hususan kupitia Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii ili pendekezo hili liweze kufikiriwa kwa makini zaidi likiwa limetokana na mmojawapo wa Kamati za Bunge hili.

Lakini wazo lenyewe mimi naliona linavutia sana kwa sababu tutakuwa tunafanya jambo la uhakika kuhakikisha kwamba bajeti kwa ajili ya Elimu ya Msingi inapatikana kwa uhakika na watoto wetu waweze kufundishwa vizuri.

**MHE. AGGREY J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa jana niliuliza swali hapa Bungeni kuhusu Shule ambazo zipo katika Jimbo langu la Siha ambazo zinaonekana watoto watadondokewa na madarasa yale na Walimu mle ndani na mpango huu wa MMEM ambao unazungumzwa hapa utamalizika mwaka 2006: Je, Waziri atanihakikishia hapa kwamba kabla ya mwaka 2006 Shule hizo zitakuwa zimepewa mgao maalum kwa ajili ya kuzikarabati?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, mpango huu ni wa mwaka 2002 mpaka 2006. Ni kweli kabisa kwamba ujenzi wa madarasa ulikuwa unafanywa katika mikupuo mitatu na hivi karibuni kwenye mwezi wa Januari fedha za mkupuo wa tatu ndiyo zimetolewa.

Sasa hizo fedha ambazo zimetoka mwishoni mwa Desemba lakini mwanzoni mwa Januari, tunategemea zikafanye kazi ya kumalizia majengo ya Shule tufikie darasani kuwa na wanafunzi wasiozidi 40, lakini kwa taarifa tulizonazo katika baadhi ya Wilaya,

lengo hili linaonekana tutakuwa hatujalifikia hata baada ya kumaliza huu mkupuo wa tatu.

Kinachohitajika sasa na ndiyo ningependa kuchukua nafasi hii kutoa ushauri ni kila Halmashauri ya Wilaya kuangalia pale ambapo hawajafikia mkao sahihi wa ulishaji wa elimu ambao unahitaji darasani watoto wazisidi 40, basi waandae *mopping up project* yaani *project* nyingine ili tuweze kuwa na awamu ya nne ya kuweza kukamilisha ujenzi wa madarasa na nyumba za Walimu pale ambapo baada ya mwaka huu tutakuwa hatujakamilisha na makisio hayo yawahishwe katika bajeti hii ya mwisho kwa maana ya bajeti ya mwisho ya kupitishwa na Bunge hili ili tuweze kumalizia kazi hii nzuri tuliyokuwa tunaifanya katika kipindi hiki.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Watoto ambao wananufaika na mradi huu ambao unafadhiliwa kwa kiasi kikubwa na Wafadhili kutoka nje, sasa katika hali hii ambapo wanafunzi hawa ndiyo watakuwa Darasa la Sita mwaka ujao, Waziri anataka kuliambia Bunge hili na Taifa kwa ujumla kwamba sasa Serikali haina hata mjadala wowote na Wafadhili hawa ili kuongeza muda wa mradi huu au Serikali yenyewe haina hata mkakati wowote wa bajeti halisi ili kuendeleza mradi huu na kuwa na maana zaidi?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, Ni kweli kabisa kwamba mradi huu wa MMEM umehisaniwa sana na Wahisani pamoja na mkopo kutoka Benki ya Dunia. Hili lilihitajika kwa sababu kazi tuliyohitajika kuifanya ilikuwa ni kubwa sana. Mwaka 2000 wakati Bunge hili lilipochaguliwa, katika Shule zetu tulikuwa na wanafunzi milioni 4,300,000 lakini sasa tuna zaidi ya milioni saba. Kwa hiyo tulihitajika kujenga madarasa kwa kiwango kikubwa sana. Lakini baada ya kumaliza utekelezaji wa mpango huu, hatutakuwa na haja ya kujenga madarasa mengi kwa kiasi hicho kwa sababu sasa uongezaji wa madarasa utaendana na kuongezeka kwa wanafunzi kwa kawaida kulingana na kuongezeka kwa wingi wa watu.

Kwa hiyo, hatuendelea kuhitaji mkopo.
Lakini ni kweli pia kwamba sehemu ya fedha za uendeshaji, ile ruzuku ya uendeshaji ilikuwa inatokana na mkopo lakini Waheshimiwa Wabunge mmesikia mara kwa mara taarifa za Serikali kwamba makusanyo ya Serikali yamekuwa yakiongezeka. Kwa hiyo tutawajibika kupanga fedha nyingi zaidi kutokana na ongezeko la makusanyo yetu ya kodi za ndani kupanga kwa ajili ya elimu.

Kwa hiyo mimi nina hakika kwamba hatimaye uendeshaji wa elimu utaweza kuhudumiwa na bajeti yetu sisi wenyewe. Endapo tutaiona haja ya kuomba misaada zaidi au kukopa hatutasita kufanya hivyo kwa sababu sisi ni Wanachama wa Benki ya Dunia na tukiwa na shida tunaweza kwenda kwa Benki ya Dunia kukopa kama tutatimiza masharti.

**Na. 79**

**Shule za Awali**

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Elimu ya Awali ni muhimu katika uboreshaji wa Elimu ya Msingi; na kwa kuwa hiki ni kipindi ambacho watoto wenye vipaji maalum wanaweza kutambuliwa na kwa kuwa utaratibu wa Serikali ni kuwa kila palipo na Shule za Msingi iwepo na Shule ya awali:-

(a) Je, shule hizo za awali zinawajibika kwa nani na ni nani anahakiki ubora elimu inayotolewa?

(b) Je, vipo Vyuo vingapi nchini vinavyotoa mafunzo ya Ualimu wa kufundisha Shule za Awali na ni nini hatma ya baadaye ya Walimu hao muhimu katika nchi yetu?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ireneus Ndunguru Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utafiti umeonyesha kuwa Elimu ya Awali ni muhimu sana katika maendeleo ya Elimu ya mtoto. Mtoto asipoandaliwa vizuri katika kipindi cha miaka sita ya mwanzo, madhara yake katika kujifunza hudumu katika maisha yake yote. Mtoto akipewa elimu bora ya awali huweza kusoma vizuri zaidi anapoanza Shule ya Msingi. Elimu hii ni muhimu kwa sababu:-

(i) Inapunguza utoro na kurudiarudia madarasa;

(ii) Inaongeza ubora wa Elimu inayopokelewa na mtoto;

(iii) Inarahisisha kazi za Walimu katika kufundisha hasa katika Darasa la Kwanza na la Pili; na

(iv) Inarahisisha utumiaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Kutokana na umuhimu huo, Wizara yangu kupitia Sera ya Elimu na mafunzo ya mwaka 1995, imetoa maelekezo kuwa kila penye Shule ya Msingi iwepo na Shule ya Awali kwa watoto wa miaka mitano na sita.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Ireneus Ndunguru Ngwatura, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mageuzi ya Serikali za Mitaa *(Local Government Reforms),* uanzishwaji, ujenzi na umiliki wa Shule za Msingi na Shule za Awali ni wa jamii husika. Wizara yangu inawajibika katika kutoa Miongozo ya Kisera,

kuandaa Mitaala, kuandaa Walimu wa Shule hizo na kuzikagua ili kuhakiki ubora wa elimu itolewayo.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kukidhi mahitaji ya Walimu wa Shule za Awali, Wizara yangu ilitenga Vyuo vya Ualimu vya Mpwapwa, Kitangali, Songea, Butimba, Singachini, Tabora na Kasulu ili kutoa mafunzo ya mwaka mmoja kwa Walimu wa Daraja la 'A' waliopo kazini. Ili kuongeza wigo wa mafunzo kwa Walimu wa Shule za Awali, Wizara yangu kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania imeandaa upya mihutasari kwa Walimu wanaosomea Daraja la III A. Kwa hiyo, kuanzia mwaka 2005. Vyuo vyote vya Ualimu vitafundisha taaluma hii ya Elimu ya Awali kwa Wanachuo wote wanaochukua mafunzo ya Daraja la IIIA kwa kupitia masomo mawili yaitwayo:-

(i) Malezi ya Elimu ya Awali; na

(ii) Mbinu za kufundisha Elimu ya Awali.

Kwa hiyo, kila Mwalimu anayehitimu atakuwa na angalau na ujuzi huo.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika majibu yake amesema kwamba Elimu ya Awali ni muhimu sana na liko tatizo hasa katika maeneo ya Vijiji ambavyo kusema ukweli hizi Shule bado hazipo na kama zipo ni za ubabaishaji:-

(a) Je, Serikali inaweza ikatoa umuhimu kama ule iliyoutoa kwenye mpango wa MMEM ?

(b) Kwa kuwa kuna Vyuo ambavyo vinaendeshwa sasa hivi na Mashirika ya binafsi kama vile Mashirika ya Dini kwa mfano Mbinga; Je, Serikali iko tayari kuvisaidia Vyuo hivi angalau kutoa ruzuku ili viweze kuendesha mafunzo haya ya Walimu ya Awali?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, Katika swali la kwanza Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba Shule hizi za Awali hazipo kwa ukamilifu ni kama kwa ubabaishaji, nasikitika kusikia taarifa hiyo. Inawezekana hivyo ndivyo kwa hali ilivyo huko Mbinga na katika baadhi ya sehemu nyingine sasa kama kumekuwa na kukwama katika Wilaya fulani naomba tutaarifiane ili tuone Wizara inaweza kusaidia vipi.

Mpaka sasa hatujaona haja kwamba jambo hili la Shule za Awali lisimamiwe tofauti na utaratibu niliousema kwamba ni jukumu la jamii husika. Maana yake ni kusema kwamba ni jukumu la Halmashauri za Wilaya lakini kama jambo hili tutaendelea kuliona lina upungufu.

Wizara yangu inaweza kuangalia tunavyoweza kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na wenzetu wa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tuone kama ipo haja ya kuandaa mpango wa Kitaifa wa kuimarisha Shule hizi. Kwa hiyo hili ni jambo la kuweza kushauriana zaidi.

Kuhusu swali la pili, kama nilivyomwelewa kuna Chuo cha Ualimu kinachoendeshwa na Shirika, siyo cha Serikali. Kama tungeweza kukipa ruzuku ili kiendeshe mafunzo, mimi ushauri ambao ningependa kutoa ni kwamba watumie mitaala hii tuliyoiandaa upya ambapo Mwalimu anayesomea Daraja la IIIA atajifunza na yale masomo mawili ya ziada ambayo nimeyasema. Kwa kufanya hivyo, Walimu wanaowafundisha wataweza kuyajua masomo hayo.

Mheshimiwa Spika, kama kuna haja ya Chuo hicho kupewa ruzuku hilo ni jambo tunaloweza kuzungumza, lakini napenda Mheshimiwa Mbunge na wenye Chuo hicho wafahamu kwani walipoomba kusajiriwa kuna mahali waliandika na kuweka sahihi kwamba wanao uwezo wa kifedha wa kuendesha mafunzo hayo ya Ualimu na ndiyo maana tuliwaruhusu. Sasa kama wamekwama tunawakaribisha tuongee.

**Na. 80**

**Mishahara ya Wafanyakazi Wetu katika Balozi**

**MHE. Dr. WILLIAM F. SHIJA** aliuliza: -

Kwa kuwa, thamani ya Dola ya Marekani imekuwa ikishuka kwa kipindi kirefu sasa dhidi ya Sarafu nyingine duniani na kwa kuwa kuna watumishi wa Tanzania hususan katika Balozi zetu wanapokea mishahara yao na kuendesha kazi zao kwa Dola za Kimarekani:-

(a) Je, mpaka sasa watumishi hao wanapunjika kiasi gani tangu dola ya Kimarekani kushuka thamani?

(b) Je, Serikali imefanya nini kurekebisha hali hiyo ili watumishi wa Tanzania walioko nje ya nchi wasipunjike na kuzorotesha utendaji wao wa kazi kutokana na hali hiyo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Shija Mbunge wa Sengerema, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba thamani ya Dola ya Kimarekani imekuwa inashuka dhidi ya sarafu nyingine duniani kwa kipindi kirefu sasa. Ni kweli pia kwamba watumishi wanaofanya kazi katika Balozi zetu huko nje wanalipwa mishahara yao kwa Dola ya Kimarekani.

Aidha, ni kweli vilevile kwamba kutokana na kushuka kwa thamani watumishi wa Balozi waishio katika nchi za sarafu inayoongezeka thamani dhidi ya Dola ya Kimarekani kama vile *Euro* ya Umoja wa Ulaya, *Yen* ya Japani, *Pound Sterling* ya Uingereza au *Rand* ya Afrika Kusini wamekuwa wanajikuta wana uwezo mdogo wa kimapato ikilinganishwa ilivyokuwa kabla ya thamani ya Dola kushuka.

Kwa kutambua ukweli wa tatizo hilo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Hazina tumekuwa na utaratibu wa kufidia pengo. Kadhalika, kuanzia Oktoba mwaka wa jana Wizara imekuwa inawapelekea watumishi waliopo katika nchi mbalimbali mgao wao kwa sarafu ya nchi hizo. Utaratibu huu umesaidia kupunguza tatizo kwa muda wakati tunatafuta jawabu la kudumu la tatizo hili.

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Kwa vile tumeimarisha Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki na sasa hivi tunatarajia kuingia katika mpango wa kufanya biashara ya pamoja kwa nchi hizi tatu:-

Je, Serikali haioni ni muda muafaka sasa wa kuwa na sarafu inayolingana kwa nchi hizi tatu badala ya kuwa na hela tofauti kwa nchi hizi tatu ili wafanyabiashara wetu watakapoanza kufanya biashara hizi waweze kutumia hela hiyo moja yaani sarafu inayolingana?

**SPIKA:** Ni swali zuri lakini ni jipya. Kwa hiyo, bora ulilete katika utaratibu wa kawaida, ila kama Mheshimiwa Waziri unaweza kuliarifu Bunge juu ya jambo hilo, basi endelea. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hadija Kusaga, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo.

Katika ujenzi wa Umoja wa Afrika Mashariki, tumekubaliana tutajenga umoja wetu hatua kwa hatua. Hatua ya kwanza ni Umoja wa Forodha ambao sasa hivi ndiyo tumeanza kuanzia tarehe mosi Januari, mwaka huu 2005. Hatua ya pili ni soko la pamoja ambapo sasa kutatokea ruksa kwa watu kuweza kuishi katika nchi yoyote ya Afrika Mashariki bila kizuizi na kufanya kazi. Hatua ya tatu ni Umoja wa Sarafu na hatua ya nne ni Shirikisho la kisiasa.

Kwa hiyo, kuwa na sarafu ya pamoja ni katika malengo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini hatua ambazo zimekwishachukuliwa mpaka sasa kurahisisha wafanyabiashara ni kitu tunachokiita *convert ability of currencies* kwamba sarafu za nchi zetu hizi tatu zinaweza kutumika katika nchi yote hii bila ya vikwazo. Kabla ya hapo ni kwamba kama ukiwa unakwenda Kenya mfanyabiashara lazima uende kwenye Benki upate dola ama fedha yoyote ya kigeni halafu ukishatoka pale unakwenda Kenya unaingia Benki unapata fedha ya Kenya ndipo ufanye biashara lakini makubaliano yaliyokuwepo ni kwamba unaweza kuchukua Shilingi ya Tanzania ukaenda nayo Kenya, ukaenda kwenye Benki ukabadilisha ukapata pesa za Kenya na ukafanya biashara bila ya kikwazo.

Kwa hiyo, hili limerahisisha ufanyaji wa biashara katika kipindi cha sasa. Lakini hilo linakuja na sarafu ya pamoja na kuna mapendekezo ya kuharakisha, kuongeza kasi ya hatua hatua hizi mbalimbali tuone hapo itakapokuwa imekubaliwa pengine tutachukua muda mfupi zaidi kufikia kwenye sarafu ya pamoja kuliko ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

**Na. 81**

**Itifaki ya Ushuru**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR (k.n.y. MHE. FATMA SAID ALI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Itifaki ya Ushuru wa pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki ilikamilika na kusainiwa mwezi Machi, 2004 kwa lengo la kuimarisha biashara na kukuza uchumi wa nchi husika:-

Je, Watanzania wameandaliwa vipi kukabiliana na zoezi hili jipya?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali ma Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mbunge wa Mlandege, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Itifaki ya kuanzisha Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ilitiwa saini mwezi Machi mwaka jana 2004 na kuanza kutekelezwa rasmi mwezi Januari mwaka huu baada ya kuridhiwa na Mabunge ya nchi wanachama. Pamoja na mambo mengine, Umoja wa Forodha umeweka viwango sawa vya Ushuru wa Forodha yaani *Common External Tariff* kwa bidhaa kutoka nje ya nchi za Afrika Mashariki ili kuendeleza viwanda vya ndani ya Jumuiya. Pia, nchi wananchama zimekubaliana na utaratibu wa kuondoleana viwango vya ushuru wa forodha kwa biashara ya ndani. Kwa utaratibu huo, bidhaa za Tanzania na Uganda zitaingia kwenye Soko la Kenya bila ushuru wa forodha, wakati bidhaa kutoka Kenya kwenda Tanzania na Uganda zitaondolewa ushuru kwa utaratibu maalum kwa muda wa miaka mitano tangu kuanza kwa utekelezaji wa Itifaki. Ili kutekeleza kwa ufanisi utaratibu wa kuondoleana ushuru wa forodha, nchi wanachama zilikubaliana juu ya vigezo vya kuhakiki uasili wa bidhaa *(Rules of Origin)* zitakazonufaika na utaratibu wa kuondoleana ushuru wa forodha ndani ya Jumuiya.

Mheshimwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Said Ally, Mbunge wa Mlandege kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata manufaa ya kushiriki katika Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Serikali inaendelea na mikakati ya kuboresha sera na kulenga katika kuboresha mazingira ya uzalishaji na biashara nchini. Hatua hizo ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Kuwashirikisha wadau wengi kwenye mchakato mzima wa majadiliano na makubaliano ili kujenga ufahamu na kuwa wamiliki wa maamuzi yaliyofikiwa.

(ii) Baada ya Mikataba kuwekwa saini na kuanzwa kutekeleza rasmi sheria, kanuni na taratibu mbalimbali zilichapishwa na kusambazwa ikiwa ni pamoja na kuingizwa kwenye Tovuti ya *TRA*. Aidha, Semina mbalimbali zilifanyika mwaka jana na mwaka huu kuhamasisha na kupanua uelewa wa wadau mbalimbali kuhusiana na suala hili.

(iii) Kuboresha mfumo wa leseni za biashara ili kuondoa kero kwa wafanyabiashara. Serikali imefuta ada ya leseni kwa biashara zenye mauzo yasiyozidi Shilingi milioni 20 kwa mwaka na kuweka kiwango cha ada cha Sh. 20,000/= kwa mauzo yanayozidi Shilingi milioni 20 kwa mwaka.

(iv) Kuweka Mfuko wa Dhamana ya Mikopo kwa ajili ya Wauzaji wa Bidhaa Nchi za Nje yaani *Export Credit Guarantee Scheme.*

(v) Kuanzisha Mfuko wa kudhamini mikopo ya Sekta ya wenye Shughuli Ndogo Ndogo za Kibiashara *(Small and Medium Enterprises)* chini ya usimamizi wa Benki Kuu kwa kushirikiana na Shirika la kuhudumia viwanda vidogo *(SIDO).*

(vi) Mpango na mkakati wa kufuta kodi baina ya nchi wanachama umetoa muda wa miaka mitano kwa bidhaa 880 ambazo zitaendelea kupata ulinzi ili kuhakikisha ushindani halali na ulinzi wa viwanda vyetu.

(vii) Kuanzisha program ya kusajili rasilimali isiyotambulika rasmi ili iweze kutambulika na kutumika kama dhamana kwa lengo la kusaidia wananchi kupata mitaji kutoka vyombo vya fedha kwa ajili ya kuendeleza miradi yao.

(viii) *TRA* imeanzisha *Inter-Bank Settlement System*, utaratibu ambao umeshaanza kutumiwa na wafanyabiashara wakubwa na unatarajiwa kutumika kwa walipa kodi wote.

(ix) Maandalizi yako katika hatua za mwisho kuwezesha waagizaji na wasafirishaji nje kutuma kadhia zao kwenye Ofisi za Forodha kwa njia ya mtandao wa *Computer - Direct Trader Input (DTI).*

(x) Mwisho, Idara ya Forodha imeanza kutumia *Computerized Risk Management System* ili kuondokana na utaratibu uliokuwepo wa kukagua kila shehena. Hii ni pamoja na matumizi ya *X-ray Scanner* katika Bandari ya Dar es Salaam kwa nia ya kuwezesha mizigo kuondoshwa kwa haraka.

**Na. 82**

**Barabara ya Mbeya - Kapalala/Kininga**

**MHE. PAUL E. NTWINA** aliuliza:

Kwa kuwa Serikali ina mipango mizuri ya kuunganisha barabara ya Wilaya kwa Wilaya, Mkoa kwa Mkoa, Vijiji kwa Vijiji na kwa kuwa sehemu ya barabara ya Kapalala - Gua imebaki kuwa ya Wilaya na baada ya hapo ile ya Gua - Mpanda hakuna barabara ambayo ingekuwa rahisi sana kufikia Mikoa ya Tabora na Kigoma kwa kupitia Mpanda ambayo ni fupi sana:-

(a) Je, Serikali inajua barabara hii ilikuwepo wakati wa Ukoloni ingawa sasa imefutika?

(b) Je, Serikali kwa kuacha kufikiria kutengeneza barabara hiyo, haioni kuwa ni sawa na kuwaweka wananchi kwenye kisiwa ambapo barabara haipitiki na hakuna mawasiliano ya karibu ya Kiwilaya/Kimkoa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:

Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Paul Ntwina, Mbunge Songwe, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kuwa barabara za Mbeya - Saza - Mkwajuni hadi Makongolosi yenye urefu wa kilometa 118 na Saza hadi Kapalala yenye urefu wa kilometa 57.0 ni barabara za Mkoa zinazohudumiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara, Mkoa wa Mbeya. Barabara kutoka Kapalala hadi Gua ni barabara ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya. Kutoka Gua hadi Mpanda hakuna barabara, kuna pori/msitu ambao ni Hifadhi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Ntwina, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara yangu haina kumbukumbu yoyote inayoonyesha kuwa palikuwepo na barabara kati ya Gua na Mpanda wakati wa Ukoloni ambayo sasa imefutika.

(b) Ni kweli hakuna barabara kati ya Gua na Mpanda na hili ni eneo la Hifadhi ya Taifa. Endapo Mheshimiwa Mbunge bado anaona kuna umuhimu wa kufungua barabara hii, ninamshauri Mheshimiwa Mbunge kuwasilisha mapendekezo haya kwa Halmashauri za Wilaya husika ili mradi huu uweze kupitiwa na kuingizwa katika mipango yao ya maendeleo ya Kimkoa.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, majibu yamekuwa turudi tena katika Halmashauri kujadili hili, nina swali kama ifuatavyo, kwa kuwa, kuna umuhimu wa eneo hili kufunguliwa kwa sababu kuna mbuga za wanyama na pia kuna eneo ambalo kulikuwa na mgodi wa almasi ule wa Ngwala na kwa kuwa kutokuwepo na barabara kunafanya hili eneo lidumae katika uchumi wa nchi hii. Je, hilo Waziri atasema nini? Hawezi kushirikiana na Wizara ya Maliasili wakatengeneza eneo la barabara hizi ninazozisema? Hilo ni swali la kwanza.

La pili ni kwamba, kati ya barabara ya Saza kwenda - Kininga - Kapalala ambayo ni ya *TANROAD* ambayo ni ya kwake Waziri kama alivyokubali haipitiki wakati huu wa mvua hasa maeneo yale ya Kidongo Chekundu na Kidongo Cheusi, sasa licha ya ahadi je hawezi kulitengeneza hili eneo likapitika kwa muda wote?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kufungua barabara mpya kunahitaji kuwepo na mipango na ndiyo maana nilimshauri Mheshimiwa Mbunge apeleke kwenye Halmashauri ili Halmashauri ikikubali ipeleke kwenye Kamati ya Ushauri ya Mkoa halafu iende kwenye *Road Board* ya Mkoa ili ione kama kuna haja ya kufungua hiyo barabara na vile vile labda niseme tu waombe Wizara ya Maliasili na Utalii waone kama watapata ruhusa ya kuingia kwenye msitu huo na kutengeneza barabara.

Ile barabara ya Saza - Kapalala sehemu ya Kidongo Chekundu na Kidongo Cheusi ni sehemu ngumu na Mheshimiwa Mbunge anaijua inahitaji pesa nyingi sana kutengeneza kwa sababu ya ugumu wake. Tunajitahidi ili iweze kupitika, lakini mara nyingine wakati wa mvua nyingi tunashindwa kuifungua ipitike kabisa. Lakini tutaendelea kujitahidi.

Na. 83

**Ujenzi wa Nyumba za Ghorofa Mjini (Jijini) Dar es Salaam**

**MHE. MOSSY S. MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa majengo mengi ya ghorofa yanayojengwa Jijini Dar es Salaam yamedhihirika kutokuwa na sifa zinazokidhi viwango:-

(a) Je, Serikali imetoa uamuzi gani kuhusu majengo hayo yasiyo na viwango vinavyotakiwa?

(b) Je, katika zoezi la ukaguzi wa majengo hayo ni mangapi yaliyokosa sifa?

(c) Je, *"Construction Engineers"* wa majengo hayo wamechukuliwa hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mossy S. Mussa, Mbunge wa Mfenesini, swali lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Serikali inatambua umuhimu wa ubora wa majengo yanayotakiwa kutumiwa na wananchi wake. Kwa kutambua hilo, Serikali imeunda asasi za majengo kama ifuatavyo:-

(i) Bodi ya Usajili ya Wasanifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi *(Architects and Quantity Surveyors Registration Board);*

(ii) Bodi ya Usajili wa Wahandisi *(Engineers Registration Board);*

(iii) Bodi ya Usajili wa Makandarasi*(Contractors Registration Board);* na

(iv) Halmashauri za Miji.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inahusika moja kwa moja na Mamlaka ya asasi tatu kati ya nne nilizozitaja hapo juu, yaani *AQSRB, ERB na CRB*. Kulingana na kumbukumbu ama takwimu tulizonazo kutoka *ERB, AQSRB* na *CRB*, Jijini Dar es Salaam hakuna majengo ya ghorofa yaliyodhihirika kutokuwa na sifa zisizokidhi viwango vilivyopo kama swali la Mheshimiwa Mossy linavyodai.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria Na. 17 ya mwaka 1997 ya Usajili wa Makandarasi, inapotokea kuwa majengo yanayojengwa Jijini Dar es Salaam hayana sifa zinazokidhi viwango hususan majengo ya ghorofa na yale ambayo ni kwa ajili matumizi ya umma, Wizara yangu, kupitia Bodi ya Usajili wa Makandarasi *(CRB)* huchukua hatua zifuatazo:-

Pale ambapo ujenzi umefanywa bila kutumia Mkandarasi aliyesajiliwa kwa mujibu wa Sheria, ujenzi husimamishwa mara moja na kumshtaki mtuhumiwa katika vyombo vya dola au kumlipisha faini isiyopungua asilimia kumi ya thamani ya mradi au Sh. 5m/= au kifungu cha miaka mitatu au vyote kwa pamoja, yaani kulipa faini na kufungwa miaka mitatu

Mkandarasi aliyesajiliwa na Bodi akifanya ujenzi bila kuzingatia ubora na usalama wa kazi, hupewa adhabu mbalimbali kulingana na kosa ikiwa ni pamoja na kupewa onyo, kulipishwa faini, kusimamishwa kufanya ujenzi kwa muda au kufutiwa usajili.

Katika kipindi cha mwaka 2001 na mwaka 2003, jumla ya miradi 1,066 ilikaguliwa. Kati ya hiyo, miradi 151 (asilimia 19) ilijengwa bila kutumia Kampuni zilizosajiliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi, wakati miradi 426 (asilimia 52) haikuzingatia usalama wa kazi.

Aidha, Makandarasi 1,449 walifutiwa usajili, 96 walisimamishwa *(suspended)* kufanya shughuli za ukandarasi na 175 walilipishwa faini kwa makosa mbalimbali.

Vile vile, jumla ya wawekezaji *(clients)* 65 wamefikishwa katika vyombo vya dola kwa kujenga wenyewe bila kutumia Makandarasi waliosajiliwa.

Aidha, jumla ya Kampuni tano za Ushauri na wataalam 26 walifutiwa usajili na Bodi ya Usajili wa Wasanifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi. Vile vile Bodi ya Usajili wa Wahandisi ilisimamisha usajili wa Mhandisi Mshauri mmoja, Kampuni moja ya Ushauri ilipewa miezi mitatu ya uangalizi na *Professional Engineers* watano walipewa

onyo kali. Hadi sasa hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa dhidi ya wasiofuata taratibu kwa ushirikiano baina ya wadau mbalimbali ikiwa ni *AQSRB, CRB,* Halmashauri za Manispaa hasa Jiji la Dar es Salaam.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha. Kwa hiyo, tunaendelea na mambo mengine, kwanza ni matangazo ya vikao kwa leo. Zipo Kamati tatu; Kamati ya Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Dr. Malecela anaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane chumba Na. 231, ghorofa ya pili, mara baada ya kipindi cha maswali.

Halafu Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Haroub Masoud anaomba Kamati ya Maendeleo ya Jamii ikutane leo saa saba mchana katika ukumbi Na. 133, ghorofa ya kwanza na Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana pamoja na Naibu Waziri wanakaribishwa kuhudhuria kikao hicho.

Kamati ya Fedha na Uchumi Mwenyekiti wake anawaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa tano asubuhi hii chumba Na. 37, ghorofa ya pili. Mwisho wa matangazo ya vikao.

Waheshimiwa Wabunge naomba nitoe taarifa mapema kwamba kesho ndio tumepanga shughuli ya kuweka jiwe la msingi la ukumbi mpya wa Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote watashiriki, lakini ratiba tutawagawia baadaye na shughuli itakuwa kati ya saa nane na nusu na kumi na nusu.

Kwa leo Muswada uliopo mbele yetu una wachangiaji watano (5) tu mpaka sasa. Kwa hiyo, kama bado kuna mwenye nia ya kuchangia Muswada huo, orodha bado ipo wazi.

Mwisho wa matangazo, Katibu endelea na *Order Paper. (Makofi)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria inayoanisha Majukumu na Kazi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2005

***(The Attorney General (Discharge of Duties) Bill, 2005***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria uitwao *The Attorney General (Discharges of Duties) Act, 2005* kama ulivyobadilishwa kwa mujibu wa orodha ya

mabadiliko ulioambatanishwa kwenye orodha ya shughuli za leo, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, nina hakika Waheshimiwa Wabunge wanatambua kwamba Serikali ni chombo kinachopata uhalali wake kwa kufanya kazi zake kwa kufuata Katiba, sheria, kanuni na taratibu zenye nguvu ya kisheria. Katiba yetu imeunda Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuipa jukumu la kuishauri Serikali katika masuala yote ya Sheria. Kwa ajili hiyo Ibara ya 59 inatamka kwamba: "Mwanasheria Mkuu ndiye atakuwa mshauri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya mambo yote ya Sheria na kwa ajili hiyo atawajibika kutoa ushauri kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuhusu mambo yote ya sheria na kutekeleza shughuli nyingine zozote zenye asili au kuhusiana na sheria zitakazopelekwa kwake au zitakazoagizwa na Rais kuzitekeleza na pia kutekeleza kazi na shughuli zinginezo zilizokabidhiwa kwake na Katiba hii au sheria yoyote.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu wakati nikiwasilisha Muswada wa Mabadiliko ya Kumi na Nne ya Katiba, Serikali inaendelea kufanya mabadiliko kwa ajili ya kuboresha sekta ya sheria na mfumo mzima wa utoaji haki nchini. Mapendekezo yaliyomo katika Muswada huu yalifanyika baada ya uchambuzi wa kina wa matatizo yanayoikabili sekta ya sheria kuhusu mfumo, miundombinu na utendaji.

Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyobainishwa na upembuzi huu na ambayo inapendekezwa kuyatatua yanahusu, kwanza mfumo wa kutoa ushauri wa sheria Serikalini na pia mfumo wa kuendesha mashtaka nchini.

Mheshimiwa Spika, upembuzi uliofanywa umeonyesha umuhimu wa kuboresha mfumo wa kutoa ushauri wa sheria Serikalini kwa kuweka utaratibu madhubuti unaomwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kusimamia jukumu lake la kutoa ushauri wa sheria Serikalini sasa hivi. Kanuni B(9) na B(10) za kanuni za kudumu za utumishi zinaelekeza Idara za Serikali kupata ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika mazingira yafuatayo:-

(a) Kabla ya Serikali kuamua kulipa fidia ya aina yoyote.

(b) Kabla ya Ofisa wa Serikali hajatoa ushahidi wa nyaraka za Serikali Mahakamani.

(c) Kabla ya kupeleka shauri lolote la jinai Mahakamani.

(d) Kuihusisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika mchakato wa kuandaa Miswada ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, hayo ni baadhi tu ya masuala ya kisheria ambayo Mwanasheria Mkuu wa Serikali anatakiwa kuyatolea ushauri. Baadhi ya Wizara na Idara za Serikali zimekuwa zikiajiri Wanasheria na Washauri Sanifu *(Consultants)* na kutumia

ushauri wao moja kwa moja bila ya kumhusisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kutokana na kukosekana kwa utaratibu huo wakati mwingine Mwanasheria Mkuu wa Serikali amekuwa akifuatwa tu pale matokeo ya ushauri uliotolewa bila kumhusisha yanapokuwa yamesababisha Wizara au Idara au Taasisi kufikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unakusudia kutatua tatizo hilo. Muswada huu unapendekeza kuweka utaratibu utakaoziwezesha Idara, Wizara na Taasisi za Serikali kupata ushauri katika mambo yote ya kisheria au yenye asili ya sheria ama kutoa moja kwa moja kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali au kwa utaratibu unaomwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kujua na kuratibu ushauri huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu pia unakusudia kuainisha utaratibu wa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kumsaidia Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuimarisha mfumo wa kusimamia mashtaka nchini kwa kuimarisha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Muswada huu unapendekeza mambo yafuatayo:-

(a) Kuweka utaratibu utakaomwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kusimamia kikamilifu jukumu la kutoa ushauri wa sheria Serikalini.

(b) Kuainisha majukumu ya Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kazi za kila siku za ofisi yake.

(c) Kuainisha wajibu wa Wanasheria wanaotoa ushauri wa sheria waliopo katika Wizara, Idara na Taasisi nyingine za Serikali katika kazi za kila siku za ofisi zao.

(d) Kuelezea majukumu na utaratibu wa Mkurugenzi wa Mashtaka, kusimamia mashtaka, kuweka vigezo vitakavyomwongoza atakapofanya maamuzi ya kufungua mashtaka, kuingilia kati mashtaka yanayofunguliwa na watu binafsi na kusitisha mashtaka ya jinai. Marekebisho haya pia yatafungua njia kwa utekelezaji wa uamuzi wa Serikali wa kutenganisha kabisa uendeshaji mashtaka na zile za upelelezi ili hatimaye kazi ya kuendesha mashtaka ifanywe chini ya usimamizi kamili wa Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu nne na kuna nyongeza. Sehemu ya kwanza ni ya utangulizi. Inatamka jina la Muswada utaratibu wake wa kuanza kutumika pamoja na tafsiri ya maneno mbalimbali yatakayotumika katika sheria.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, ina maelezo ya msingi ya shughuli za Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Majukumu haya kimsingi ni yale yale yaliyotamkwa katika Katiba. Sehemu hii inaanzisha utaratibu wa kutekeleza majukumu hayo ambapo Mwanasheria Mkuu wa Serikali anatakwa kuwa na mamlaka ya kuiwakilisha Serikali katika mashauri yote katika Mahakama zote kwa mujibu wa sheria ya mashauri dhidi ya

Serikali ya Mwaka 1967 au kesi iliyofunguliwa na mtu yeyote ambayo inahusu maslahi ya Serikali au kama maslahi ya umma yanahitaji Serikali iingilie kati.

Pili, inaweka utaratibu utakaowezesha kesi zinazofunguliwa katika Mahakama ambazo Mwanasheria Mkuu au Mawakili wa Serikali hawaruhusiwi kufanya kazi, kuhamisha kwenye Mahakama zinazoweza kufanya kazi na mwisho kuweka utaratibu utakaomwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwasimamia na kuwaelekeza Wanasheria waliopo katika Ofisi za Serikali nje ya Ofisi yake.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii vile vile inaelezea namna Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakavyowajibika kwa Mwanasheria Mkuu katika kusimamia majukumu mbalimbali yatakayotekelezwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu, inaelezea kazi mbalimbali zitakazotekelezwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwanza sehemu hii inahusu Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye ndiye Msimamizi Mkuu wa Mashtaka nchini. Aidha, sehemu hii inaeleza majukumu yake ya kusimamia mashtaka bila kuingiliwa, kusimamiwa nidhamu ya Mawakili wanaoendesha mashtaka na kusimamia upelelezi unaohusu kesi anazoziendesha. Sehemu hii inaelekeza uhusiano wa Mkurugenzi wa Mashtaka na Mwanasheria Mkuu wa Serikali hususan kuhusu mambo ya sera na utawala wa Mawakili kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii vile vile imeainisha majukumu mengine ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya kuishauri Serikali, Idara na Taasisi zake katika Mikataba ya Kibiashara *(contract)* na Mikataba mingineyo ya Kimataifa *(treaties),* masuala ya Katiba na haki za binadamu, utayarishaji wa Miswada ya Serikali pamoja na shughuli mbalimbali za Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu ambaye pia ni Msajili Mkuu wa Serikali *(Registrar General),* Mdhamini wa Serikali *(Public Trustee)* na *Official Receiver.*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne, inaelezea utaratibu wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kusimamia ushauri wa sheria unaotolewa na Maofisa walio nje ya ofisi yake. Inapendekezwa kwamba Wanasheria wataendelea kuajiriwa katika Wizara, Idara na Taasisi nyingine za Serikali watakaojulikana kwa kazi zao kwa kadri ajira zao zitakavyoruhusu kama vile Maofisa Ardhi, Wasajili wa Hati, Watafiti wa Sheria, Wanasheria wa Halmashauri, hao wanaofanya kazi za utawala, Maofisa wa Fedha wa Hazina na kadhalika. Inapendekezwa kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali awe na uwezo wa kuwateua maofisa hao kufanya kazi ya Mawakili wa Serikali katika sehemu zao. Watakaoteuliwa watawajibika moja kwa moja kwake.

Aidha, inapendekezwa kwamba hata baada ya kuwateua Maofisa hao bado Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakuwa na haki yeye mwenyewe kutekeleza moja kwa moja majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano, inapendekeza utaratibu mahsusi wa kutoa ushauri katika Serikali za Mitaa kupitia Wizara inayohusika na Serikali za Mitaa kwa kuzingatia uhuru wa Serikali za Mitaa katika kufanya maamuzi yake.

Serikali hizo zinaruhusiwa kuwa na Wanasheria wao ambao kwa kawaida huitwa *Municipal Solicitors* au *City Solicitors au Town Solicitors* kufuatia hadhi ya Taasisi husika.

Hata hivyo kutokana na ukweli kwamba wote hawa watakuwa wanatekeleza shughuli za kisheria na Kikatiba ipo haja ya kuweka utaratibu unaotumika katika kutekeleza majukumu yao.

Hivyo basi, inapendekezwa kwamba katika Wizara inayohusika na Serikali za Mitaa kuwe na Maofisa Wanasheria watakaoratibu ushauri unaotolewa katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita, inaainisha taratibu za kumwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kusimamia utekelezaji wa kazi za kutoa ushauri wa sheria Serikalini na inapendekezwa kwamba Mwanasheria Mkuu atasimamia ushauri Serikalini kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuelekeza kuhusu mambo ya Katiba, Mikataba ya Kimataifa na mambo mengine yatakayotajwa mahsusi katika sheria yatatolewa au ushauri kwa idhini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mwenyewe.

(ii) Uajiri wa Washauri Sanifu katika masuala ya Sheria utafanywa kwa kibali cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali mwenyewe. *(Makofi)*

(iii) Mwanasheria Mkuu atatoa maelezo ya kiutendaji kwa Wanasheria wa Serikali wanaofanya kazi ya Serikali.

(iv) Kubainisha wazi kwamba ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu jambo lolote la sheria utakuwa ndio msimamo wa kisheria wa Serikali. Ofisa yeyote wa Serikali atakayefanya maamuzi kinyume chake atawajibika.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii vile vile inaainisha utaratibu wa kupata ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba ya Muswada huu, inapendekeza utaratibu wa ajira ya Wanasheria wa kuwakabidhi majukumu ya Uwakili wa Serikali. Mwanasheria Mkuu wa Serikali atawateua Wanasheria wanaofaa kutekeleza majukumu yake na ni hao tu ndio watakaofanya kazi ya Uwakili wa Serikali.

Vile vile inapendekezwa kwamba, liwepo daftari la Mawakili wote watakaopewa mamlaka ya kufanya kazi ya Uwakili wa Serikali. Sehemu hii pia inaelekeza kuwepo kanuni ya maadili ya Mawakili. Kanuni zinazopendekezwa zimeainishwa katika

nyongeza *(schedule)* na Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakuwa na uwezo wa kuzibadilisha kila mara haja ya kufanya hivyo itakapojitokeza.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nane, inapendekeza kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali. Kwa kuwa mapendekezo yaliyopo katika Muswada huu yanagusa sheria mbalimbali ipo haja ya kuzifanyia marekebisho sheria hizo ili zioane na sheria hii ili kutekeleza mabadiliko yanayopendekezwa:-

(i) Sheria ya Mawakili inafanyiwa marekebisho ili kuwezesha *Solicitors* walioajiriwa katika Halmashauri watambulike kama Mawakili.

(ii) Sheria ya Serikali za Mitaa Na. 7 na 8 za Mwaka 1982 zinafanyiwa marekebisho ili kuainisha majukumu ya Wanasheria wanaofanya kazi katika Halmashauri waweze kufanya kazi za kutoa ushauri kwa Halmashauri.

(iii) Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka ya Jinai pia inafanyiwa marekebisho ili kuainisha utaratibu wa Wanasheria waliopo katika Halmashauri kuendesha mashtaka katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanayopendekezwa yana lengo la kuhakikisha kwamba Serikali yetu inakuwa na utaratibu bora kabisa wa kupata ushauri wa kisheria na hivyo kufanya maamuzi kwa mujibu wa sheria. Jambo hili litafanya Serikali iwajibike vizuri zaidi kwa kufuata Katiba na sheria za nchi. Bila shaka tunakubaliana kwamba Muswada huu ni nyenzo muhimu ya kudumisha utawala wa sheria nchini.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wayatafakari mapendekezo haya ya Serikali na kuyaafiki.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI (k.n.y. MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBU, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala juu ya Muswada wa Sheria ya Utekelezaji wa Kazi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2005 *(The Attorney General (Discharge of Duties) Bill, 2005).*

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa wakati wa kikao cha Kamati hii tarehe 24 Januari, 2005 Kamati ilipata fursa ya kupokea mapendekezo ya Serikali

yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na pia kusikiliza maoni ya mdau Dr. Sifuni Mchome, Mkuu wa Idara ya Sheria za Madai na Jinai kutoka Kitivo cha Sheria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi kwa mujibu wa kifungu Na. 70(2) cha Kanuni za Bunge, Toleo la 2004 na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, naomba nichukue nafasi hii kutoa maoni ya Kamati katika maeneo kadhaa ya,Muswada huu baada ya kutafakari kwa kina.

Mheshimiwa Spika, nikianza na ya jumla ni kwamba kimsingi Kamati inaunga mkono Muswada huu ambao nia yake ni kumwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuongoza na kuweka utaratibu utakaomwezesha kuishauri Serikali vizuri akisaidiwa na Wasaidizi wake katika taasisi na maofisa wengine katika Taasisi, Idara na Wizara za Serikali. *(Makofi)*

Muswada huu utaziba pengo la muda mrefu la kutokuwepo kwa utaratibu ambao ungemwezesha Mwanasheria Mkuu kuishauri Serikali vizuri na kwamba unakwenda sambamba na mabadiliko yaliyofanyika katika Ibara za 59(a) na 59(b) kwa mujibu wa mapendekezo yaliyomo katika Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya kumi na nne ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, lingine la jumla ambalo Kamati inapenda kulieleza ni wasiwasi juu ya kuwajibika kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kitaaluma, Wanasheria walioko katika maeneo mengine ya Serikali kama Wizara, Halmashauri za Wilaya na kadhalika wakati huo huo wakitakiwa kuwajibika kiutumishi kwa waajiri wao.

Kwa kuzingatia kuwa mamlaka za ajira za Wanasheria hawa zinatofautiana pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kutaka kuwa mfumo mzuri wa kuishauri Serikali toka Asasi na Taasisi mbalimbali za Serikali kwa kuziunganisha na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kamati inashauri kuwa Serikali ihakikishe kuwa utaratibu huu hautagonganisha mamlaka mbalimbali za ajira za Wanasheria hasa pale Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakapotaka kumchukulia hatua Mwanasheria atakayekiuka maadili ya taaluma yake.

Mheshimiwa Spika, lingine la jumla linahusu kutambuliwa kwa nafasi za Mkurugenzi wa Mashtaka katika Katiba. Kwa kuwa nafasi hii imetambuliwa Kikatiba na kwa kuzingatia majukumu makubwa aliyonayo Mkurugenzi wa Mashtaka Kamati inashauri kuwa katika siku zijazo Serikali ifikirie kuzitenganisha Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Mashtaka Kiutendaji na siyo kisera ili kumwezesha Mkurugenzi wa Mashtaka kumiliki vyombo vilivyo chini yake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo pia kwa kuwa Kurugenzi za Mashtaka ni nyingi, basi ni vyema jina lake liwe Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai ili aweze kutofautishwa na wanaosimamia mashtaka ya aina nyingine kama mashtaka ya madai na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya tafsiri Kamati ilishauri kuwa Kabidhi Wasii Mkuu aliyetajwa katika Ibara ya 13 ya Muswada huu na Mkurugenzi wa Mashtaka aliyetajwa katika Ibara mbalimbali za Muswada wajumuishwe katika sehemu ya tafsiri katika Ibara ya 3 ya Muswada huu. Nafurahi kuwa Serikali imezingatia ushauri huu kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho lililowasilishwa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwenye Ibara hiyo ya 3 Kamati ilikuwa na mjadala mkali juu ya tafsiri mbili za kada za Maafisa wa Sheria waliotajwa katika tafsiri. Kada hizo *Law Officers na Legal Officers.* Kuhusu *Law Officers* imeelezwa kuwa tafsiri yake ni kama ilivyo katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria Toleo lililojadidiwa la mwaka 2002 yaani *the Interpretation of Laws and general crosses Act revised addition 2002.*

Katika sheria hii *Law Officer* ameelezwa kuwa ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali yaani *Attorney General* na mtu yeyote mwenye sifa za taaluma ya Sheria katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mwenye cheo cha Uwakili wa Serikali Mwandamizi yaani *Senior State Attorney* au Mwandishi wa Sheria Mwandamizi yaani *Senior Parliamentary Draftsman* au Vyeo zaidi ya hivyo. Na *Legal Officer* kama ilivyo kwenye Muswada ni mtu aliyehitimu na kubobea katika sheria na kuajiriwa katika Ofisi ya Umma ukiacha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tafsiri hii pia inawahusisha Wanasheria wa Halmashauri za Miji, Manispaa au Wilaya yaani *solicitors.*

Mheshimiwa Spika, tafsiri hizi mbili kama nilivyoeleza zilizua majadiliano makali kwa jinsi zilivyofanana na kwamba yalikuwepo mapendekezo kuwa tafsiri ya *Legal Offficer* iondolewe kwani haikuwa na sababu kuwepo. Hata hivyo, baada ya kuangalia kwa kina Kamati ilishauri kuwa tafsiri ya *Legal Officer* iboreshwe zaidi na kuonyesha walau awe na kiwango cha chini cha Shahada ya Sheria na awe mtu ambaye amebobea katika sheria yaani *Legally Qualified Personal or Graduate in Law.* Hili limezingatiwa na Serikali na limo katika jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 5 ya Muswada Kamati inaafiki mantiki iliyoelezwa katika Ibara ya kumfanya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa Wakili namba moja awapo Mahakamani kwa mujibu wa wadhifa wake. Hata hivyo, Kamati haiafiki dhana ya kuwapa wadhifa kama huo baadhi ya Mawakili watakaomwakilisha Mahakamani. Kamati imezingatia kuwa katika Mahakama kuwepo Mawakili wa siku nyingi na isingekuwa busara wazee kama hao kuongozwa na vijana wadogo wanaomwakilisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hivyo basi, Kamati inashauri kuwa ni pale tu Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Naibu wake watakapofika Mahakamani wao wenyewe ndiyo wapewe wadhifa wa kuwa Wakili namba moja na Wakili namba mbili kwa mujibu wa nyadhifa zao kiofisi. Kwa sababu hiyo Kamati ilishauri kuwa Ibara ya 5(3) iandikwe upya. Kwa bahati nzuri ushauri huu nao umezingatiwa kwa kiasi kikubwa kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa sehemu kubwa ya shughuli za Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kushauri. Kamati haikuona mantiki ya yeye kupewa

jukumu la kutafsiri na kutoa maana ya sheria zilizotungwa na Bunge yaani *to interpret and find meaning out of parliamentary enactments,* kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 8(j). Kamati inashauri kuwa kifungu hiki kirekebishwe na jukumu hili lihusishwe katika kuishauri Serikali tu yaani *to advise the Government on the interpretation* ya sheria na kadhalika. Aidha, kwa kuwa mapendekezo yaliyopo katika Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya kumi na nne ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano yamelenga kumpa uhuru mkubwa Mkurugenzi wa Mashtaka. Kamati haioni mantiki kuifanya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iwe mdhibiti wa mashtaka yote ya jinai nchini kama inavyopendekezwa katika Ibara ya ndogo za 8(1)(a)na (b). Kamati inashauri vifungu hivi vifutwe.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 11 ya Muswada inamlazimisha Mkurugenzi wa Mashtaka kupokea maelekezo ya kisera na kiutawala kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kamati ilitafakari kwa kina pendekezo hili na kuona kuwa akishalazimika kupokea maelekezo hayo hasa ya kiutawala Mkurugenzi wa Mashtaka kamwe hatokuwa uhuru na madhumuni yote ya kuifanya Kurugenzi hiyo ijitegemee hayataonekana. Kwa sababu hiyo Kamati inashauri kuwa apokee maelekezo ya kisera tu na kwamba aendelee kuwa uhuru isipokuwa kuwe na chombo cha kufuatilia kazi zake kwa utaratibu kuwa awe anawajibika Bungeni ama moja kwa moja au kupitia kwenye Kamati ya Bunge inayohusika na Sheria. Kwa utaratibu huu atawajibika kuwasilisha taarifa zake Bungeni zijadiliwe.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa Ibara ya 14 iandikwe upya kwa kuweka maneno *Director Responsible for Constitutional Affairs and Human Rights* hii ni kuzingatia kuwa Kurugenzi hii tofauti na nyingine zilizotajwa katika Ibara hii yaweza kubadilika wakati wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Kamati ilijielekeza ni katika Ibara ya 17 nayo inahusu Haki ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya kushiriki Mahakamani kama kuna kesi yoyote inayohusu maslahi ya umma yaani *Public Interest.* Kamati imetafakari haki hii. Hata hivyo, imeona kuwa maneno ya maslahi ya umma yanaweza yakatumiwa vibaya na Serikali. Hivyo ili kulinda haki za binadamu Kamati inashauri kuwa Ibara hii irekebishwe kwa kuondoa maneno hayo na badala yake iachiwe Mahakama iamue kama suala hilo ni maslahi ya umma au hapana.

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo maeneo ambayo Kamati yangu imeyatolea maoni. Aidha, yapo mengine ambayo Serikali iliyatolea ufafanuzi na Kamati yangu iliridhika. Yale ambayo sikuweza kuyagusia natumaini Wajumbe wa Kamati hii watayajazia watakapopata fursa ya kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati. Pia napenda nimshukuru Mheshimiwa Andrew Chenge, Mbunge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalam wake wote kwa kutoa maelezo yao kina mbele ya Kamati na kuiwezesha Kamati ielewe madhumuni na malengo ya Muswada huu bila matatizo.

Vilevile namshukuru Dr. Sifuni Mchome mdau kutoka Kitivo cha Sheria Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kutoa maoni yake ambaye yameisaidia sana Kamati katika kuishauri Serikali hususan katika eneo la Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mwisho kabisa, napenda niwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa kuwa makini wakati wote tulipochambua Muswada huu na kutoa michango ya mawazo ambayo imesaidia sana kuuboresha Muswada huu tofauti na ulivyokuwa katika hatua zake za awali.

Naomba niwatambue kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Athumani Janguo Mwenyekiti, Mheshimiwa George Malima Lubeleje Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Khamis Salum Ali, Mheshimiwa Ramadhani Khalfan, Mheshimiwa Juma N'hunga, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na mwisho ni Dr. Masumbuko Lamwai. Nawashukuru pia Makatibu wa Kamati hii Ndugu Ernest Zulu, Charles Mloka na Aggrey Nzowa kwa kuihudumia vyema Kamati na kutayarisha maoni ya Kamati mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wa Spika kwa kutumia kifungu cha 55(3).

Mheshimiwa Spika, jana tulilalamika na naona tunazidi kulalamika. Sasa hotuba ya Waziri ukilinganisha na *schedule of amendment* karibu zinalingana ziko kurasa 6. Je, tunataka kujua na labda tunaomba mwongozo wako kwa siku zijazo hata kama siyo kwa leo. Tunafanya nini tunapoletewa makaratasi mengi namna hii wakati tunatakiwa kwenda kutoa hoja yetu kuhusu hoja iliyotolewa na kama mabadiliko ni mengi kiasi hiki maana yake tunachoenda kutoa kwa kweli hakina uhusiano na kile ambacho kimeshafanyiwa kazi na Serikali. Tutakuwa tunafanya kazi ambayo haina maana.

Vilevile tunajua kwamba katika kifungu cha 70 kazi hii inatakiwa iletwe na *Order Paper* angalau inatupa muda wa saa moja na nusu wakati wa kipindi cha maswali kuifanyia kazi. Sasa katika hali hii kwa kweli tunafanya kazi ambayo haina tija yoyote na haina manufaa kwa sababu tumeletewa hapa na hata karatasi ukizishika bado zina moto.

Sasa mimi sijui ni nani anayehusika zina moto kwa sababu zimetoka kwenye *photocopy.* Sijui anayehusika ni nani, lakini mimi suala siyo anayehusika ni fulani. Suala nitufanyie angalau Bunge na Wabunge haki waweze kujadili yanayofanyika na

yanayozungumzwa humu ni mambo mazito japo yanaonekana madogo. Ukibadilisha *folio* kwa kisheria ni jambo nzito sasa mpaka uende kuangalia *folio* kwenye *Principle Legislation* inasema nini. Sasa tusipofanya kazi hii tunapitisha vitu ambavyo hatujafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hata mimi umenivamia sasa sijapitia vizuri hizo kanuni ulizozitaja. Lakini ninachojua moja kwa moja ni kweli mabadiliko yoyote yanatakiwa yaambatanishwe na *Order Paper* ya siku hiyo. Haya makablasha tuliyopewa leo ni kweli hayakuambatanishwa pamoja na *Order Paper* yamekuja tumeshamaliza kipindi cha maswali. Kwa hiyo, tuseme mmecheleweshwa kwa muda wa saa moja na nusu kuyaona. Lakini kama hilo ndiyo tatizo, basi nitachelewesha muda wa kuingia kwenye Kamati ya Bunge Zima. Maana yake haya marekebisho huwa yanashughulikiwa wakati wa Kamati ya Bunge Zima siyo kabla. Kwa hiyo, kama hivyo ndivyo nitachelewesha baada ya Muswada kusomwa mara ya pili hatutaingia Kamati ya Bunge Zima moja kwa moja ili Waheshimiwa Wabunge mpate nafasi ya kutafakari hayo marekebisho yaliyotolewa. Ahsante sana. Sasa Kambi ya Upinzani maoni Mheshimiwa Kiongozi wa Shughuli za Upinzani Bungeni.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE - KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na Muswada wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali *(The Attorney General (Discharge of Duties Act, 2005)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(b) na 81(1) kuhusu Muswada ulioko mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unatokana na Mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara ya 59 ambayo inaanzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa Mshauri Mkuu katika Masuala ya kisheria. Lengo la Muswada ni kuainisha majukumu na kazi za Mwanasheria Mkuu, uhusiano wa Mwanasheria Mkuu na Wanasheria waliopo katika Wizara na Taasisi za Serikali na kumpa mamlaka Mwanasheria Mkuu kutoa maelekezo kwa Wanasheria wanaofanya kazi Serikalini na katika Taasisi za Umma kuhusu utaratibu wa kutoa ushauri Serikalini. Pamoja na nia hii nzuri, Kambi ya Upinzani inapenda kutoa maoni yake kutokana na Ofisi inayoundwa kwa Sheria hii kuwa Ofisi nzito sana. Tunagusia tu maeneo yafuatayo, kwa uchache:-

Kwa kutafakari sifa na utaalamu wa Mwanasheria Mkuu kama inavyotolewa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake, na hasa Ibara ya 59(2) ikisomwa pamoja na Ibara ya 118, yaani sifa zinazofanana na za Jaji wa Mahakama ya Rufani, na kwa kuzingatia kazi zake kama zilivyofafanuliwa. Kambi ya Upinzani inakubaliana kabisa na hoja ya wadau kuwa Mwanasheria Mkuu ni mtaalamu anayepaswa kuwa amebobea katika mambo ya Kisheria, anayepaswa kutoa ushauri wake kwa Serikali bila ushabiki wowote wa kisiasa, wala kuegemea upande

wowote wa kisiasa, anatakiwa asiwe Mwanasiasa, ili ushauri wake uweze kusimamia utaalamu tu. Kwa msingi huo tunaamini inawezekana kabisa, Mwanasheria Mkuu, akaingia katika Baraza la Mawaziri kama mtaalamu chini ya viapo vyote vinavyotakiwa, na akaingia pia Bungeni kama wanavyoingia watu wengine wasio Wabunge, yaani Katibu wa Bunge na Makatibu wasaidizi. Hii itamfanya Mwanasheria Mkuu kutoa ushauri uliojikita katika Sheria na utaalamu bila kujali maslahi ya kisiasa ya Chama chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, isitoshe, kama walivyo Majaji, Mwanasheria Mkuu naye anatakiwa asiwe mwanachama wa chama cha Siasa, ili kutoa ushauri wake kwa Bunge bila kuegemea au kuwa na maslahi yeyote ya kisiasa. Kambi ya Upinzani inaamini kabisa, kama kuna utashi wa kisiasa hili linawezekana kabisa ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea kutokana na Mwanasheria kutoa ushauri uonaokuwa mwelekeo wa kisiasa.

Mheshimiwa Spika, sote tunakumbuka madhara yaliyopatikana Bunge hili liliposhauriwa siku moja kwamba Wajumbe wote wa Chama fulani cha Siasa kujiuzulu katika Kamati ya Kudumu ya Bunge, kwa lengo tu la kuwaondoa Wenyeviti waliochaguliwa na Wajumbe chini ya utaratibu halali. Uamuzi ambao hatimaye, ulibatilishwa na Mheshimiwa Spika, kwa kuwateua tena Wajumbe hao hao. Tukio hilo ni dogo sana, lakini tunaweza kujikuta katika hali mbaya zaidi siku moja. Ni vema kukinga kuliko kutibu. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanyia kazi kwa kina suala hili, na kwa wakati muafaka mabadilko yanayotakiwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Sheria mbalimbali na Kanuni za Bunge zifanyiwe marekebisho ili zimruhusu Mwanasheria Mkuu kufanya kazi zake kisheria katika Baraza la Mawaziri na ndani ya Ukumbi wa Bunge. Kama kuna utashi wa kisiasa tunaamini hakuna lisilowezekana.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani vile vile inakubaliana na wadau waliopendekeza kuwa kwa vile nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni nzito sana katika nchi. Mwanasheria Mkuu ndiye anayeishauri Serikali katika masuala yote ya Sheria. Sheria hii inayopendekezwa inazidi kutoa mamlaka makubwa zaidi kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa maana kuwa ndiyo inayoandaa Mikataba yote ya Kimataifa ambayo nchi yetu inaingia, kuishauri Serikali kuhusu mambo yote ya Katiba na Haki za Binadamu; utoaji wa ushauri kwa Idara zote za Serikali, kuiwakilisha Serikali katika Mahakama zote nchini, isipokuwa mahakama za mwanzo. Haya ni mamlaka mazito sana. Mamlaka haya yako katika kifungu cha 8(1)(a) hadi (k).

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu nchi yetu na wananchi kwa ujumla tulivyoathirika kutokana na mikataba mibovu mathalani Mkataba kati ya Serikali yetu na *IPTL* ambao umesababisha Serikali yetu kulipa kila mwezi wastani wa shilingi bilioni 3.5. Sote tunafahamu kutokana na Mkataba mbovu jinsi Shirika la *TTCL* lilivyouzwa kwa bei ya kutupwa kutokana na kutokuwa waangalifu katika maandalizi ya Mkataba wa awali. Kuna mifano mingi tu ya aina hiyo ambayo lazima wakati ufike kuwa mtu anayesimamia mikataba hiyo, hatimaye awajibike kwa Bunge.

Hivyo, ili kusimamia utekelezaji wa Mamlaka hayo makubwa, Kambi ya Upinzani inapendekeza Mwanasheria Mkuu, akiisha kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, athibitishwe na Bunge, na uwajibikaje wake uwe kwa Bunge badala ya kuwajibika kwa Rais. Pendekezo hili lina nia ya kuimarisha usimamizi wa utendaji kazi katika Ofisi nyeti kama ya Mwanasheria Mkuu. Kuthibitishwa kwa Mwanasheria Mkuu si jambo jipya, kwani kuna nchi kadhaa zinafuata mfumo huo kufuatana na uzito wa Ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Manunuzi, *The Public Procurement Act,* nayo inamwongezea Mwanasheria Mkuu majukumu hata katika maeneo ambayo huko nyuma hayakumhusisha kisheria Mwanasheria Mkuu. Kutokana na Sheria ya *Public Procurement Act,* Mikataba ya ununuzi wa vifaa upitiwe na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kama sote tunavyofahamu, manunuzi yanachukua zaidi ya asilimia 70 ya Bajeti ya maendeleo. Hivyo, si vema mikataba mikubwa kiasi hiki kinachochukua zaidi ya asilimia 70 kuachiwa chini ya Ofisi ambayo haiwajibiki moja kwa moja kwa Bunge.

Ni kweli kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ndiye anayekagua Mahesabu ya Serikali. Lakini sote tunafahamu kuwa ukaguzi huo unaletwa Bungeni na au kwenye Kamati husika ya Bunge kama *Postmorte m*tu. Ndiyo maana katika mikataba yote iliyozusha utata hakuna hatua yeyote iliyoweza kuchukuliwa kwa vile hatimaye watu wengine wameondoka kazini, wengine wamefariki, lakini hata ofisi yenyewe iliyohusika kupitisha mikataba hiyo haiwezi kuwajibishwa kwa vile haiwajibiki kwa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa misingi iliyotajwa, basi iwapo hoja hiyo itakubalika, Kambi ya Upinzani haina tatizo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupewa majukumu ya kuwa Mshauri Mkuu wa Serikali katika mambo yote ya Sheria kama inavyopendekezwa katika Muswada huu. Kambi ya Upinzani inahitaji kupata maoni ya Serikali kwa kina kuhusu mapendekezo haya, na lini yanaweza kuanza kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 10 kinamzungumzia Mkurugenzi wa Mashitaka ya Jinai, *(Director of Criminal Prosecution).* Kambi ya Upinzani inapendekeza Mkurugenzi wa Mashitaka asiwe chini ya Mwanasheria Mkuu. Mkurugenzi wa Mashtaka amekabidhiwa majukumu makubwa yanayohusiana na Mashtika ya Jinai. Huyu ndiye anayesimamia watumishi wote walioko chini ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, anaratibu shughuli zote za upelelezi.

Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai amepewa majukumu ya kuingilia kesi yoyote yenye maslahi ya umma na kuwa na haki ya kuondoa kesi katika hatua yeyote kutumia haki yake ya *"Nolle Prosequi."* Kambi ya Upinzani inadhani hoja siyo tu kuwa na Ofisi inayojitegemea ya Mkurugenzi wa Mashitaka, lakini pia Ofisi hii inatakiwa iwajibike kwa Bunge, kwa Bunge kuthibitisha uteuzi wake, kuwe na muda maalum wa utumishi na

akiisha kuteuliwa asiondolewe isipokuwa kwa sababu maalum zilizoainishwa kwenye sheria na kwa utaratibu maalumu.

Hii itamfanya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai kufanya kazi zake kwa uhakika na kwa kujiamini bila kuogopa na kujali kuingiliwa kupitia maslahi yake binafsi.

Mheshimiwa Spika, tunaelewa nia ya Serikali kumwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa na mamlaka na madaraka ya kisheria ya kuratibu Wanasheria wote katika Wizara, Idara na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani inaitahadharisha Serikali kuwa mwelekeo wa kuweka mamlaka yote chini ya chombo au mtu mmoja ni hatari na ni kinyume cha dhana yote ya kupeleka madaraka ngazi za chini, hasa kwa mamlaka za Miji na Halmashauri za Wilaya na Manispaa.

Kwa muda mrefu sasa nchi yetu imekuwa ikiendesha warsha na semina nyingi chini ya Programu ya Maboresho. Katika Sheria hii kifungu cha 24(3) Mwanasheria Mkuu anatakiwa kuwateua kwa hati inayotolewa chini ya mkono wake. Anayekuteua kwa kawaida ndiyo mkubwa wako na uwajibikaji lazima uelekee kwake, pamoja na kuwa wataendelea kulipwa na Mkurugenzi husika au Katibu Mkuu wa Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, hatua hii ya kuwaweka Wanasheria wote chini ya Mwanasheria Mkuu isipodhibitiwa vizuri inaweza kuhatarisha hatua zote zilizochukuliwa chini ya maboresho, lakini pia kuua moyo katika vyombo hivyo vya chini.

Hatua hiyo pia inaweza kusababisha usumbufu na ucheleweshaji mkubwa wa mashauri ya Wizara na vyombo hivyo ambavyo sasa kwa sheria hii vinatakiwa kuwa na mawasiliano na Mwanasheria Mkuu kabla ya kuchukua hatua yeyote kwa niaba ya Serikali.

Kambi ya Upinzani inatahadharisha kuwa nia njema ya uratibu isije ikazaa balaa kubwa la umangimeza, *(red tape)* na kuingiza hasara na gharama kubwa inayotokana na athari hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 21(3) isipoangaliwa vizuri pia inaweza kuwa na madhara badala ya kuwa na manufaa. Mwanasheria Mkuu au Naibu wake amepewa mamlaka ya kutoa maelekezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya kisheria kwa Wanasheria walioko katika Wizara, Idara zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali ya Mitaa.

Watumishi hawa kimsingi wanatakiwa kutekeleza maelekezo ya Wakuu wao wa kazi mahali palipo kulingana na mahitaji muhimu ya sehemu husika, ikiwa ni pamoja na kesi mbalimbali zinazofunguliwa dhidi ya vyombo hivyo. Kwa Sheria hii mpya lazima kwanza wapokee maelekezo kutoka kwa Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu hata sasa kesi nyingi zinavyochelewa kwa vile faili husika ziko kwa vile uchunguzi haujakamilika au ziko kwa mkurugenzi wa mashitaka ya jinai *DPP*.

Kwa kifungu hiki badala ya kutafuta ufumbuzi kwa ucheleweshaji huu ambao umekuwa jambo la kawaida, kana kwamba hiyo haitoshi tunaongeza tena mlolongo mpya ambao kwa hakika matokeo yake ni ucheleweshaji. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo ya kina itaweka Safeguards gani ili mawasiliano haya kati ya wanasheria wa maeneo yanayojitegemea na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu yataweza kuharakishwa vipi ili haki isiendelee kunyongwa kutokana na ucheleweshaji usiyo wa lazima.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa tumetoa maoni yetu Kambi ya Upinzani pamoja na kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na *schedules of amendments* ambayo imeletwa dakika chache kabla hatuwasilishi maoni yetu tunarudia tena kukushukuru wewe binafsi kwa kutupa nafasi ya kutoa maoni haya na tunapenda kumpongeza kwa namna ya pekee Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuandaa Muswada huu na Miswada mingine iliyokwisha wasilishwa hapa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, wasemaji wangu ni Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala, Mheshimiwa Philip S. Marmo, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia muswada huu muhimu uliyo mbele yetu. Naomba nianze kwa kusema kwamba naunga mkono Muswada huu mia kwa mia. Naunga mkono Muswada huu kwa sababu kwanza unasaidia kuboresha mfumo wa kutoa haki lakini vile vile unatofautisha upelelezi na uendeshaji wa mashtaka.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi wananchi wengi wamekuwa wakilalamikia Mahakama kwamba zinachelewesha kesi lakini tatizo kubwa lichangiwa na Mahakama zenyewe kuchelewesha kesi. Tatizo kubwa na sugu na ambalo kwa bahati mbaya haliongelewi na hakuna anayeonekana kulitilia shaka ni upelelezi usiyokwisha ambao mara nyingi umekuwa ukichangia kesi kutoenda kwa kasi inayotarajiwa.

Lakini muswada huu ni kwa bahati nzuri umetofautisha upelelezi pamoja na mashtaka na kwa sababu hiyo utasaidia sana kila mtu kuwajibika na kama kesi itachelewa tutaweza kujua ni nani hasa ana sababisha kuchelewesha kwa kesi husika.

Lakini vile vile Muswada huu utatoa ajira kwa vijana wetu wengi wanaomaliza katika vyuo vikuu mbalimbali na kwa sababu hiyo leo hii Bunge hili linapopitisha muswada huu si tunaboresha sheria lakini vile vile tunatengeneza ajira kwa vijana wetu wengi waliyomaliza kwenye vyuo vikuu na ambao hawana ajira. Kwa hiyo, ni matarajio yangu Mheshimiwa Rais atau-*sign* haraka muswada huu ili basi wale ambao nafasi zinazotengenezwa na muswada huu waweze kupata ajira. Lakini pamoja na hayo ninayo

maelezo ambayo ningependa Mheshimiwa Waziri ajaribu kuyatizama na aone kama anaweza kuyafanyia kazi kwa nia ya kuboresha muswada huu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kifungu cha 8 sehemu ya kwanza na kifungu cha 10 (1) na kifungu cha 11 (2) ukiviangalia vifungu hivi kwa pamoja vinaonyesha kwamba kuna haja ya kufanya marekebisho ya *Criminal Procedure Act* ya mwaka 1985 yaani sheria ya mwenendo wa mashitaka. Lakini nasikitika kwenye *schedule* ya sheria ambazo Mheshimiwa Waziri ametaja kwamba zitarekebishwa sheria hii ya *Criminal Procedure Act* ya mwaka 1985 haijatajwa kwamba na yenyewe itafanyiwa marekebisho.

Kwa hiyo, ningependa nishauri kwamba ni vizuri na sheria hiyo iongezwe kwenye sheria zile zitakazofanyiwa marekebisho kwa sababu kama sheria hii tunayotunga leo tukitaka ifanye kazi basi lazima na *Criminal Procedure Act* ya mwaka 1985 ifanyiwe marekebisho. Kwa nini nasema ifanyiwe marekebisho. Ifanyiwe marekebisho kwa sababu moja kubwa *Criminal Procedure Act* inampa madaraka *Director of Public Prosecutions* wakati sheria mpya inaondoa madaraka hayo kwenda kwa Ofisi ya *Attorney General.*

Mheshimiwa Spika, kama hivyo ndivyo ilivyoilivyo basi lazima ukimwondolea madaraka ukayapeleka kwa *Attorney General* basi lazima uende kwenye sheria ya *Criminal Procedure Act* ya mwaka 1985 uifanyie marekebisho ili sheria hii iweze kufanyakazi kama ambavyo tunakusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini wakati sheria hii inajaribu kumpa madaraka *Attorney General* ya kuratibu mashitaka ya jinai yote katika nchi kwa kuangalia kifungu cha 8 (1)b vile vile inaleta utata ukiangalia kifungu cha 11 (2) kwa sababu kifungu cha (1)b kinaeleza kwamba *Attorney General* atakuwa *overall* katika masuala ya jinai katika nchi lakini vile vile ukienda kifungu cha 11 kinasema *Director of Public Prosecutions (DPP)* atakuwa *overall* katika masuala yote ya *Prosecutions.*

Mheshimiwa Spika, naomba hapa kwa wataalam wetu na Mheshimiwa Waziri anisaidie kuliweka sawa ni nani ana madaraka ya mwisho ni *Director of Public Prosecutions* kama inavyoonekana kwenye kifungu cha 11 sehemu ya 2 au ni *Attorney General* kama inavyoonekana kwenye kifungu cha 8 sehemu ya 1 (b).

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile utata unaojitokeza kwenye kifungu cha 10 (2)a na kifungu cha 10 (3) urekebishwe kwa sababu vinapingana. Kwa nini vifungu hivi vinapingana, ukiangalia kifungu cha 10 (2) kinaeleza kwamba *DPP* ataweza kukaimisha madaraka yake kwa *Law Officers,* Wanasheria wa Serikali na wengineo imeelezwa pale. Lakini ukienda kifungu cha 10 (3) kinaeleza vile vile kwamba *DPP* atawakilisha Serikali kwenye *Criminal Appeals filed in High Court na Court of Appeal* sasa swali hapa je, itakuwa lazima *DPP* mwenyewe kujiwakilisha *in person* kwenye *High Court* na kama italazimika hivyo tutakuwa tunachelewesha kesi kwa sababu *High Court* inaweza ikawa na vikao vya kesi kwa siku wanaweza wakakaa Arusha, wanaweza wakakaa Mwanza, wanaweza wakakaa Bukoba, wanaweza wakakaa Dar-es-Salaam.

Sasa ukiwa na sheria inayosema lazima *DPP* mwenyewe aende *in person* basi utakuwa unaleta mazingira ya kuchelewesha kesi kwa sababu wa Mwanza watasema kesi hii haiwezi kuendelea kwa sababu *DPP* hawezi kuja kwa kesi hii kwa sababu yupo Dar-Es-Salaam. Lakini ukiangalia kifungu cha 10 (2)a kilijaribu kuondoa hilo kwa kueleza kwamba *DPP* ataweza ku-*delegate* madaraka yake, lakini ukija kwenye kifungu hiki kinamtaka kwenye *Court of Appeal* na *High Court* awepo yeye in *person.* Sasa ningeomba huo utata urekebishwe ili tusije tukatengeneza sheria yenye vifungu vinavyopingana vyenyewe kwa vyenyewe.

Mheshimiwa Spika, ukienda kifungu cha 3 (b) nadhani sheria nzuri ni pamoja na kutokuwa na maneno yanayorudiwa rudiwa ovyo ovyo bila sababu. Utaona kwamba pale wanataja, sina haja ya kusoma kwamba ukiangalia kifungu cha 3 (b) kwamba kutakuwepo *AG, a Law Officer or State Attorney* lakini kuyataja taja haya maneno kuyarudia rudia haina sababu. Kwa sababu ukienda kwenye *definition* ya *AG* kwenye utangulizi tayari tumesha sema ukitaja *AG* maana yake unataja *Law Officers* na *State Attorney,* sasa si vizuri kurudia rudia mambo na ndiyo maana kwenye uandishi wa sheria tunajitahidi kuwa na *definitions.* Ukishakuwa na *definitions* kwamba hiki kinamaanisha hiki huna sababu kwenda ndani ya muswada kuanza kurudia mambo yale yale.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kifungu cha 3 (d) vile vile utakuta kwamba tunasema kwamba huyu *AG* anaweza aka-*file certificate* kwenye *Court* ya kujaribu kuomba kesi fulani iwe *transferred* kwenda kwenye Mahakama nyingine. Lakini swali langu hapa ninalouliza ni kwamba ingekuwa vizuri kuwamo na hivi vifungu vya muswada ili viendane na *Magistrate Court Act* ya mwaka 1984.

Mheshimiwa Spika, tatizo la sheria ni kwamba unapogusa moja lazima uwe tayari kuzigusa na sheria nyingine zinazohusiana. Sasa hapa tumeelezea tu kwamba *AG* ataweza ku-*file a Certificate in Court ya* kuomba ku-*transfer* kesi fulani kwenda Mahakama nyingine. Lakini tumesahau kuwamo na vifungu vilivyokwenye *Magistrate Court Act* ya mwaka 1984, lakini vile vile tumesahau kufanya marekebisho kwenye sheria namba 2 ambazo zinaweka muongozo wa kuhamisha kesi kutoka Mahakama moja kwenda Mahakama nyingine.

Mheshimiwa Spika, vile vile ukienda kifungu namba 6 (b) kinatoa madaraka kwa *Attorney General* yaku-*order court* kwamba *Attorney General* nitanukuu kwamba, *Attorney General may file a certificate in the Court requiring.* Mimi ugomvi wangu ni neno *requiring* kwa sababu kwa *Concept* ya *separation of powers, Attorney General* ni sehemu ya *Executive* kwa hiyo kama unajua dhana ya *separation of powers* huwezi ukatumia neno *requiring* badala yake unaweza ukasema *Attorney General may file a certificate in Court making the application ana apply siyo ana require.* Kwa hiyo, neno *requiring* maana yake utakuwa unalazimisha Mahakama badala yake anaweza aka-*apply* ili uipe uhuru wa Mahakama kutizama kwamba ombi hilo la *Attorney General* liko sawa sawa au haliko sawa sawa. Lengo ni kuhakikisha kwamba ile dhana ya *separational powers* in zingatiwa.

Mheshimiwa Spika, kama hayo niliyoyasema yatazingatiwa na ningeshauri Mheshimiwa *Attorney General* atazame kwa kina pamoja na Mheshimiwa Waziri ili basi Muswada huu tunaopitisha uendane na sheria nyingine zote ambazo zinahusiana na kile tulichokilenga. Baada ya kusema hayo naomba nirudie kwamba naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, nawasifu wachangiaji wa leo kwa kuusoma vizuri Muswada. Mheshimiwa Philip S. Marmo.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi nipate nafasi ya kujadili muswada huu. Muswada huu kimsingi hauna tatizo una ainisha na kuweka katika sheria, hali tuliyozoea ya utendaji wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ajili hiyo nilitaka kusema toka awali ni kwamba naunga mkono.

Mheshimiwa Spika, mimi sikuwa kwenye Kamati hii na siyo mjumbe wa Kamati kwa hiyo kama nitarejea yaliyojadiliwa kwenye Kamati siyo makusudi. Lakini mimi sikupata nafasi ya kuona hotuba ya Kiongozi wa Upinzani lakini kama ikionekana naongelea aliyosema kwamba imetokea tu hivyo siyo kwamba namjibu.

Nikianzia hapa nilitaka kusema kwamba muswada una ainisha yale ambayo ndiyo tuliyozoea ndiyo mazoea yetu, hivyo pengine muswada pia ungetaja pale ambapo kulikuwa na wasiwasi. Kwa mfano nafasi ya Mwanasheria Mkuu Bungeni hili ambalo wameliongelea Kiongozi wa Upinzani ushauri wake uchukuliweje. Napenda kuliongelea hili kwa kirefu kidogo, lakini pia mazoea mengine tuliyoyazoea pengine kwa nini ameachwa kwa mfano haingepaswa sasa pia kutaja kwenye sheria kama hii ile nafasi ya Naibu Mwanasheria Mkuu ya kuwa Katibu Mkuu hata kama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu itakuwa chini ya Wizara fulani baadaye.

Sasa nikirejea pengine sheria ingetaja moja kwa moja kwamba Mwanasheria Mkuu siyo Mwanasheria wa Bunge, siyo mara ya kwanza duniani kutajwa imetajwa katika maeneo mbalimbali na wasomi wamerejea eneo hili kwa kina kwa sababu hizi hizi ambazo Kiongozi wa Upinzani hapa amekuwa akilisema, na wasomi wamekuwa wakirejea sasa nafikiri katiba ya Jamaica ambayo inataja kabisa Mwanasheria Mkuu wa Serikali siyo mshauri wa Bunge kisheria. Ambao wamekuwa wakitoa maoni yao juu ya katiba hii wengine bahati mbaya wametoka angenisikiliza vizuri ningewanukuu kwa kingereza wanasema *the role of Attorney General as we all know in eyes of the public is no longer in partial as a system of justice is over leaden by Party Political considerations. So the Attorney General works for the interest of the Government and Political Party to which is affiliated,* mwisho wa kunukuu.

Kwa hiyo, hakuna sababu ya wapinzani ndani ya Bunge au nje ya Bunge kuloloma juu ya nafasi ya Mwanasheria Mkuu, ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Serikali ile ambayo inaongozwa na chama kile kwa wakati ule. Imewahi kutokea tunashangaa kuwa ameendelea kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa chama fulani

baadaye hata akaendelea kuwa Mwanasheria wa chama cha upinzani ambacho kikashika Serikali lakini ni sehemu chache.

Mheshimiwa Spika, sasa tunasema ili iwe wazi kwa sababu imetokea kwenye Bunge hili kwamba Mwanasheria amejaribu kutenda haki katika uendeshaji wa shughuli za Bunge lakini baadaye pamoja na kwamba mtiririko wa shughuli za Bunge kunatakiwa haki itendeke lakini ameweza kugeuka na hapa nataka kurejea Tume Teule ya Bunge iliyokuwa inashughulikia suala la Zanzibar kujiunga na shirika la kimataifa. Wakati ule kulikuwa ndani ya kamati Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliunga mkono taarifa ya Kamati moja kwa moja kwamba ni kinyume kabisa kwa sehemu ya Jamhuri ya Muungano kujiunga na taasisi ya kimataifa.

Lakini tulipofika Bungeni Mwanasheria huyo huyo amegeuka asilimia 100 na kuipinga kabisa taarifa ya Kamati ambayo kwa hakika ilikuwa wazi na tulikuwa tumeshangaa kwa wakati ule inakuwaje Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaunga mkono ukiukaji wa katiba. Lakini hii imetokea na ndiyo maana nimenukuu hili kwamba Mwanasheria wa Serikali anatetea maslahi ya Serikali ya chama kile. Kwa hiyo, hapa nataka kurejea kwamba maoni yake Bungeni siyo maoni yenye maana kubwa sasa na hapa ningesema kwa vile Wanasheria wote wa umma kwa namna moja au nyingine wako chini yake hii ina maana pia na Wanasheria wa Bunge? Mimi ningesema la. Nimesema hili mapema kwa sababu pia ningependa kufahamu sasa wakati huu utekelezaji wa kazi yake tukifahamu hali hii ambayo hatuikwepi ya yeye kuwa karibu na Serikali ya chama fulani. Sasa ni lini na ni wakati gani ataingilia shughuli za Mwendesha Mashitaka wa Serikali. Ni lini ingeelezwa ni lini na sheria ingetaja ni lini na wakati gani na katika mazingira yapi Mwanasheria Mkuu ataingilia utekelezaji wa shughuli za mwendesha mashitaka.

Lakini pia nini shughuli za Mwandishi Mkuu wa Sheria au shughuli za Kabidhi Wasii Mkuu, kwa ajili ya muda pengine labda nisingeenda kwa undani juu ya hili lakini ningesema tu kwamba hizi pia ni fani ndogo ndogo katika fani nzima ambazo zinaongozwa na maadili yake ni niseme labda unalielewa la uandishi wa sheria. Mwandishi wa sheria analetewa agizo au maelekezo ya kutafsiri sera iwe sheria lakini siyo mwongozi tu pengine anategemea hata dhamira yake, pengine uelewa wake wa somo au pengine nidhamu nzima ya hii fani ndogo ambayo iko ndani ya fani. Kwa vile umri nao unaenda labda mimi niseme kwa nini nimeacha kazi ya uandishi wa sheria na kujiunga yaani badala ya kuandika nikawa nimeamua niende kwenye eneo la kupitisha sheria kwa vile sasa sitarejea tena kwa umri umeenda.

Ni kwamba wakati mwingine dhamira inadai bahati mbaya Mheshimiwa Kingunge Ngombare Mwiru hayupo hapa, kuna wakati *draft instruction* kwenye ofisi ya sheria mpya ya vyama vya ushirika na *instruction* mojawapo ni kwamba sheria inatafsiri ni nini chama cha ushirika, maagizo ya Serikali ni kwamba chama cha ushirika maana yake ni kijiji, kwa fani ya uandishi w sheria kuna tafsiri ambazo lazima uwe makini kabisa mpaka uibadili kwa sababu pia kuna kubadilishana miswada hii na wenzetu wengine, nikawa najiuliza hivi ninaposema *a cooperate society is a village* wenzangu ambao tumesoma nao kutoka Uingereza, Kenya, na kutoka Botwana hivi watanielewaje? Ni kweli kwamba chama cha ushirika ni kijiji. Lakini dhamira yangu inasema kwamba

chama cha ushirika siyo kijiji, chama cha ushirika ina tafsiri pana na ya mataifa na hii ndogo haingeweza kuingia mahali popote na dhamira yangu ilikuwa inadai vile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninachotaka kusema hapo ni kwamba sasa katika hali kama hii ni lini na ni wakati gani na ni katika mazingira yapi Mwanasheria Mkuu akachukua nafasi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria ya kushika nafasi ya Kabidhi Wasii, ya kushika nafasi Mwendesha mashitaka. Ni eneo pana lakini kwa kifupi ninachotaka kusema ni kwamba fani hizi na pengine *engine* ndiyo maana kwenye Katiba tuna mwendesha mashitaka. Lingekuwa wazi kwenye sheria hii pia lini uhuru wake utawekewa vizingiti?

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya muda labda ningeenda mbele kidogo ningeachia hilo hapo ningeenda moja kwa moja kwenye shughuli au madaraka ya mwendesha mashitaka. Hili linanipa mimi taabu na wakati tukijadili Katiba kwamba hilo la katiba nililisemea ni eneo ambalo linagusa haki za binadamu ni eneo ambalo linadai pia mantiki, logic katika mazingira yetu nilishasema mahali pengine asilimia zaidi ya tisini na kitu za kesi za jinai zinaendeshwa na wale ambao wanapeleleza. Wale ambao wanawapeleka wahalifu au watuhumiwa mahabusu na kwenda kuwachukua wakati wanaotaka siyo jambo geni kwa mahabusu kuachwa kwenye mahabusu siku ambayo kesi yake inatajwa na kama Hakimu siyo makini sana akaangalia orodha ya kesi zilizopo siku hiyo na kuuliza kwa nini mahabusu fulani hajaletwa na mara nyingi kwa shughuli nyingi hawaulizi kwa hiyo watu wengi wamekaa mahabusu miezi na miaka kwa sababu ya eneo hili. Kwa sababu anayeendesha kesi ndiye anayepeleleza na ndiye anayefuatilia mahabusu na ndiyo anayeandaa na kutoa hoja ya kwamba ni wakati gani mahabusu apewe dhamana.

Kwa hiyo, mimi nadhani wakati umefika kwamba polisi wapeleleze kesi lakini uendeshaji uwe moja kwa moja chini ya Mkurugenzi wa Mashitaka. Inatia uchungu sana kwa sisi ambao tunatembelea magereza na kukuta gereza lenye kupokea watu 200 lakini 140, 160 ni mahabusu na hawana makosa ya ajabu ni vile tu polisi hawezi kwenda kumchukua angalia mahabusu kama ya kwangu pale inavyotumia wilaya nyingine polisi tena wanatakiwa wawe wawili kwenda kumchukua mahabusu kwenye jela.

Polisi akiwa mmoja kutoka Wilaya ya mbali, wilaya ambayo haina mahabusu kwa hiyo mahabusu kesi yake haiwezi kusikilizwa na hakuna atakayeuliza ni pale tu Hakimu makini, Hakimu mmoja kutaka kutenda haki aangalie orodha ya kesi zilizopo na aseme kwa nini.

Mara nyingi pale ambapo kulikuwa na hujuma wamesema kwamba leo bwana huyu hatukumleta kwa sababu ndugu zake wamejiandaa kwa sababu wakukamate kwa rushwa. Ni kitu hakipo ni kwamba tu yule bwana akae tu mahabusu kwa muda mrefu na ashike adabu na hii ni mbaya sana na imetufikisha hapa kwa sababu ya ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashitaka kutaka kubaki juu na kutokuwa na maana yoyote katika macho ya watu wengi asilimia zaidi ya 90. Kule Wilayani hivi Mkurugenzi wa Mashitaka maana yake ni nini hawamfahamu, Mwanasheria wa Serikali maana yake nini

hawamfahamu, kwa sababu hausiki na uendeshaji wa mashauri yao. Kwa ajili ya muda naomba nimalizie hapo kwa kusema tu kwamba mambo haya mengine ni ya utendaji, kwa hiyo sheria hii ikitumika vizuri bila shaka haya ninayosema yatarekebishwa. Ahsante sana.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, na mimi nakushukuru kunipatia nafasi hii lakini kwanza kabla sijaanza kuchangia nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Sheria, Mwanasheria Mkuu, Watendaji wao na Serikali kwa jumla kwa muswada waliouwasilisha na hatimaye tukaupitisha wa mabadiliko ya Katiba. Kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Mwanasheria Mkuu.

Muswada tunaoujadili ni muswada muhimu sana na muswada huu utasaidia kujenga misingi muhimu ya uongozi na hatimaye Taifa letu ili kufikia yale malengo ambayo tunayakusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uongozi wa nchi hii nafikiria vituvikubwa ambayo vinaisimamia ni Katiba na Sheria za Nchi. Mimi naamini kiongozi yeyote wa Taifa letu kama atafuata vitu viwili hivyo ataweza kuongoza Taifa hili bila matatizo yoyote, lakini kama tutashindwa sheria tunazozipitisha kuzitekeleza kwa mafanikio makubwa kuleta matumaini kwa wananchi wetu itakuwa bado hatujafanya jambo la msingi na ni hatari kwa Taifa letu.Kwa hivyo, nimtake Mheshimiwa Waziri, Mwanasheria Mkuu pamoja na Serikali kwa jumla na wananchi wote wa Tanzania kuheshimu na kusimamia Katiba na Sheria za nchi.

Mimi muswada huu unatueleza kwamba unaainisha majukumu na kazi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na nikinukuu katika Ibara ya 59 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaanzisha ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuwa Mshauri Mkuu katika masula ya kisheria. Ni jambo la msingi sana kwa sababu Serikali ndiyo msimamizi wa mambo yote yaliyomo katika nchi.

Lakini katika sehemu hii ya tatu inasema kwamba shughuli za Mkurugenzi wa Mashitaka ofisi hii itashughulika na shughuli za kutoa ushauri wa Serikali katika masuala ya katiba, madai, mikataba ya ndani na ya kimataifa, uandishi wa miswada ya sheria, haki za binadamu, kazi ya wasii na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, maeneo yote yaliyomo katika yale makusudio kwa kweli ni muhimu sana kwa Taifa letu, kwa hiyo cha msingi hapa ni Wizara na Serikali kuyatekeleza si kuyaandika.

Mimi nashukuru kwamba ushauri mkubwa sana utakuja kwenye Katiba. Sasa mimi nataka niiulize Serikali pale inapotokea watu wakavunja Katiba ya Nchi na wakashtakiwa Mahakamani na ikashindwa kupatikana uamuzi, Serikali inatoa maelezo gani kwa wananchi? Naamini ziko kesi nyingi zaidi Mahakamani. Moja ilimhusisha

labda Kiongozi wa Chama cha Siasa kwa kuikanyaga Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo, je, sheria zetu zina uzito wa kiasi gani za kumtia mtu hatiani anapofikia kufanya kitendo kama hicho ambacho naamini ni kosa la jinai. Kwa hiyo, mimi naona kwamba sheria ambayo tutakuwa tumeitunga lazima ifanye kazi na ilete faida kwa wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna madai mengine mbalimbali ya Serikali na wananchi. Sasa sijui Ofisi hii au Wizara hii yanayasimamia vipi? Kwa kweli itakapotokea wananchi wetu wakalalamika wakawa hawakuridhika na Serikali yao juu ya maamuzi waliyotoa kwa kweli tunaliweka Taifa letu katika mahali pagumu sana. Kwa hiyo, vile vile eneo hili ningeiomba Serikali iliangalie kwa mapana sana ili kuleta mafanikio na mustakabali mzuri wa Taifa letu.

Kuna manung'uniko baadhi ya mikataba ambayo Serikali yetu inaingia ni vizuri Serikali ikawa wazi kwa wananchi ili kuondoa hofu na athari moja kubwa iko kwa wenzetu ambao tunaendesha siasa za nchi hii, wanatoa maana tofauti katika kuwaambia mambo ambayo si ya kweli. Ni vizuri sisi viongozi tukawa wakweli tukafuatilia na tukafanya utafiti.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi hapa umetoa ufafanuzi juu ya Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, alilalamika kwamba kuna *paper* imewasilishwa kwamba wameshindwa hata kuingiza katika hotuba yao waliyowasilisha. Kwa hiyo, ni vizuri tujitahidi tuepushe ambayo si ya msingi tupambane na yale ya msingi na kwa nguvu za pamoja.

Vile vile kuhusu haki za binadamu. Ukitaka nchi yako sasa hivi itoke katika mfumo ambao umejipangia ni kutokea Taifa lolote likaweza kushutumu kwamba nchi ile haifuati haki za binadamu. Kwa hiyo, kama kitu hiki tumekiweka ndani ya Katiba yetu ni vizuri Serikali kuvitekeleza. Moja ni kuangalia mfumo mzima wa Mahakama zetu. Vijana wetu wengi wanahangaika Mahakamani. Kwa hiyo, ninaamini Ofisi ya Mwanasheria Mkuu itasimamia kutoa haki kwa wale wananchi ambao wako ndani ambao mpaka leo hawajapata hukumu zao ambazo kwa kweli zinawasononesha sana.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limenisimamisha hapa nimekuta katika sheria hii kuna eneo la Kabidhi Wasii. Sheria zinazoendesha eneo hili iko vipi? Mara nyingi sana kwenye Vyama vya Siasa unakuta malalamiko kwamba kuna fedha zao zimezuiliwa na Msajili wa Vyama na pengine kunakuwa na idhini pale ya Kabidhi Wasii, je, masuala kama haya tutayamaliza vipi ili kuepusha migogoro katika nchi yetu. Kwa sababu migogoro ya kisiasa si mizuri. Nchi nyingi sana zimeathirika kwa migogoro ya kisiasa na hapa pameingia na fedha kidogo. Kwa hiyo, ningelitaka Serikali iweke sheria ambayo maeneo yote haya yatafanya kazi kwa nguvu za pamoja ili kuondoa migogoro katika nchi yetu.

Tarehe 6 Februari, 2005 tulikuwa na semina hapa ambayo ilielezea kuhusu usimamizi wa maadili katika utumishi wa umma. Katika kuheshimu sheria ilikuwemo katika makaratasi waliotugawia watu wa utumishi ukurasa wa 8 kuna maeneo nataka

niyanukuu.  Inasema: “Sheria zinaweka mipaka ya madaraka, majukumu na tabia, lakini sheria zinatuongoza ili tutende kazi zetu kwa misingi ya haki na kuhakikisha kuwepo kwa usawa na amani.”

Mheshimiwa Spika, maeneo haya ni muhimu sana, sote sisi tupo hapa kwa niaba ya watu kama atakuwa ni Rais, Mahakama, Bunge au Vyama vya Siasa sote sisi malengo yetu makubwa ni kuliendesha Taifa hili kwa nguvu za pamoja kuleta umoja na amani katika nchi yetu.  Kwa hiyo, maeneo kama haya ambayo sheria inatoa ufafanuzi na malengo makubwa kuleta amani na usawa kwa Taifa letu ni vizuri tukayafanyia kazi kwa uwazi kabisa ili wananchi wote wakaweza kuelewa.  Mimi nataka niiombe sana Serikali tusifanye mzaha na masuala ambayo tumeyaandika kwenye sheria.  Tuyatekeleze kuleta faida na malengo makubwa ambayo tumeyakusudia kwa faida na maendeleo ya Taifa letu hili.

Mheshimiwa Spika, kuna sehemu moja ambayo nataka niinukuu tena.  Sehemu ya 5 inazungumzia uhusiano baina Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa.  Nataka eneo hili kama wanadamu, Serikali tuliangalie sana. Naitaka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa sababu eneo walilolishirikisha ni eneo muhimu katika Taifa letu.  Serikali ya Mitaa zinaunganisha karibu Taifa zima la Tanzania kwenye Kata,Vijiji  na maeneo mengine.  Sasa hivi inaonekana vijana wetu wengi sana wanaingia hatiani kwa kukosa kutokuelewa sheria za nchi.  Kwa hiyo, ni vizuri kwa mafanikio makubwa sana tukaweza kuweka elimu katika maeneo husika ili watu wetu waweze kujua sheria ambazo zinaweza wakaziepuka kuingia katika matatizo.

Mheshimiwa Spika, vijana wengi wanafanya mambo labda ya mchezo mchezo lakini wanapoona wamehukumiwa miaka mitano ndiyo wanajua kwamba wapo katika balaa.  Kwa hiyo, ni vizuri kama Taifa ili tuwasaidie wananchi wetu Serikali za Mitaa ichukue jukumu kuwaelimisha wananchi katika maeneo waliko itakuwa ni sehemu moja ya kuwasaidia wananchi kutokana na umaskini.  Binadamu hachungwi na mtu akienda rumande kwa siku mbili tayari amepoteza mfumo mzima wake wa maisha pale nyumbani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikachukua jukumu vile vile kutoa elimu kwa masuala ya sheria kwa yale makosa ambayo mtu yanaweza kumtia hatiani. Watu wengi wanafanya makosa wanaona ni ya kawaida lakini ni mazito.  Nataka niisaidie Serikali ione maeneo haya muhimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache nayatakia mafanikio Serikali Wizara ya Sheria na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili kusimamia majukumu haya makubwa kwa Taifa letu na wananchi kwa ujumla.  Ahsante sana na naunga mkono Muswada.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni Muswada wa kisheria na kitaaluma ya sheria. Sasa kuna mambo machache ambayo nataka kuyabaini.

La kwanza ni maeneo ya *definitions.* Kuna maneno kwenye *Additional Order Paper* kama *Legal Officer, State Attorney* na *Administration General* na mengine. Ila nina wasiwasi na neno hili *Legal Officer* wanasema *means a holder to recornise Degree.* Haya ni masuala ya utendaji, yasingekuwepo kwenye *definition.* Wangeeleza tu nafasi yake ambayo anatakiwa awe sio kueleza *qualifications.* Ni masuala ya kiutendaji ambayo wanapendekeza mtu akiwa na *Degree* mbili, *Masters* na kadhalika hayo ni masuala ya utendaji.

Baada ya hapo katika *definitions* hizo hizo kama ziliwahi kutokea kwenye sheria zilizotajwa kwa sababu sheria hii tunasema ni utawala wa kisheria. Sheria hii inaunganisha wanataaluma wanaofanya kazi za taaluma hiyo katika maeneo tofauti kuwa na kiungo muhimu ambapo wanaweza wakashirikishwa utaratibu wa taaluma yao kama ilivyo katika vyama mbalimbali vya Ualimu na maeneo mengine mengine. Lakini hii ni utaaluma wa kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, popote walipo Mwanasheria Mkuu wa Serikali alikuwa hawezi kuwaelewa kama wameajiriwa wapi. Hii kwa sababu maeneo mengi yanapata kibali kutoka Menejimenti ya Utumishi na kuajiri Wanasheria katika maeneo mbalimbali kama vile Serikali za Mitaa lakini hawawajibiki moja kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Sasa Muswada huu unaweka mtiririko ulio dhamiri kuona kwamba wanataaluma wa nchi hii ambao ni Wanasheria watakuwa sasa wanawajibika moja kwa moja kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye ndio Ofisi yao kuu. Hivyo basi maadili na utendaji kazi wao utakuwa unadhibitiwa, uhuru usiodhibitiwa unakuwa una matatizo. Uanasheria ni Uanasheria tu huwezi kuwa Mwanasheria katika maeneo mengine kwa sababu ni taasisi ukatekeleza mambo mengine bila maadili ya Uanasheria. Kwa hiyo basi, Muswada huu ukipita kwamba madaraka, kujituma, majukumu na uwajibikaji sasa yatakuwa yanajulikana dhahiri na wale watakaokuwa wanakiuka maeneo ya taaluma hii watakuwa wanadhibitiwa.

Lingine ni kwamba kwa kuwa Muswada huu unajumuisha sheria mbalimbali kama sheria namba 7 na 8 ya mwaka 1982. Sheria kama vile zilizokuwa zimeorodheshwa katika huo Muswada wenyewe. Sasa tuangalie maana na dhamira ya sheria zilizokuwa zimeoanishwa katika Muswada huu kusudi kusilete migongano ambayo Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala na Mheshimiwa Philip Marmo, aliizungumza. Kwa mfano, sheria namba 5 ya mwaka 1971, *(Marriage),* Sheria namba 12 ya mwaka 2003 kwa mfano Sheria ya *Criminal Procedure* ya mwaka 1985. Kuna maneno ya *Law Officer, State Attorney. Law Officer* wamekuwa *defined* kule *definition* za kule hazileti mgongano kwa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuangalie katika sheria mbalimbali na vipengele vinavyounganishwa kwenye Muswada huu visilete migongano. Vile vile tuangalie maeneo ya taaluma ya watu wanaokabidhiwa madaraka ya maeneo hayo katika usimamizi wao kwa uwajibikaji au katika uendeshaji wa shughuli zao kusiwe na migongano ya uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, *otherwise* Muswada huu ni kiungo muhimu kwa wanataaluma ambao wanaitwa Wanasheria ili kuwa na chombo cha usimamizi badala ya kuwa kwenye maeneo ambayo hawatambuliki na chombo kimoja cha nchi, walikuwa wamejificha wapo ingawa hawavumi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono, ahsante sana. *(Makofi)*

**MCHANGO WA MAANDISHI**

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Spika, nampogeza sana Waziri Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, kwa kuleta Muswada huu kwa wakati muafaka. Mimi nasema naunga mkono Muswada huu pamoja na hayo naomba kuchangia kidogo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kila Wizara ya Serikali na asasi muhimu ziwe na Wanasheria ili kudhibiti Serikali kuingia mikataba mibaya na kuipatia Serikali hasara.

Pili, hawa Wanasheria washirikiane kikamilifu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha kuwa mikataba na hasa ya uwekezaji na biashara inalinda maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo narudia kuunga mkono hoja hii. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya malalamiko yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani kwamba hawakupata muda wa kutosha kupitia haya marekebisho na nikaahidi kwamba nitachelewesha kuingia kwenye Kamati ya Bunge Zima. Kwa hiyo, nitamwita mtoa hoja ahitimishe hoja yake jioni ili na Kamati ya Bunge Zima ifanyike kipindi cha mchana itakuwa imekidhi mahitaji ya waliochelewa kupata orodha ya marekebisho.

Kwa maelezo haya sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.12 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, *Asalaam aleykum!*

**WABUNGE FULANI:** *Waaleykum salaam.*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii, kama ni mfululizo wa kuwasilisha hoja mbalimbali za Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Nimesimama tu kusema maneno machache ya kufafanua hapa na pale yale ambayo yana sura ya kisheria kutokana na michango mizuri iliyotolewa na baadhi ya Wabunge waliochangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitalisemea kwa kifupi sana hili la Mwanasheria Mkuu kwa sababu lina sura ile nyingine, si vizuri mimi mwenyewe nikayasema. Lakini niseme tu kwamba nafasi hii ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ilivyo kwa nchi zote zenye utaratibu huu huwa ina sura mbili. Ile sura ya taaluma ambayo ndiyo naiona msingi wake uko kwenye Katiba na sifa zake wakati Bunge lako linajadili Muswada wa mabadiliko ya 14 ya Katiba zimeainishwa kwa sababu ya kuziweka wazi zaidi lakini zimekuwepo. Kwa hiyo, ndiyo sura ya taaluma ambayo Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kama mshauri wa Serikali kwa masuala ya sheria kwa mujibu wa Ibara ya 59 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Sasa hilo ndilo la msingi sana na ndiyo maana uzito wa ofisi hii unaanzia hapo kwa sababu huyu ndiye anaishauri Serikali na vyombo vyake kwa masuala yote ya sheria. Anahitaji yeye mwenyewe awe ni mtu ambaye ana uwezo huo ana uzoefu huo, lakini nyuma yake ndiyo awe na jeshi lake lile ambalo naweza kuwaita maaskari wa miavuli wa ofisini kwake wanaoweza kuyahimili maeneo yote ambayo Muswada huu unajaribu kuyasema. Ikitetereka ofisi hii katika eneo la taaluma ndiyo unaanza kupata matatizo. *(Makofi)*

Sasa sura ya pili ya ofisi hii, ni hii ya kisiasa na ndiyo maana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ni Mbunge kwa wadhifa wake na wadhifa huo anaingia humu Bungeni, lakini anaingia katika Baraza la Mawaziri. Yeye siyo mjumbe kwa maana kwamba akifika kwenye Baraza, yeye kazi yake ni kuishauri Serikali kwamba zingatieni sheria, zingatieni Katiba, zingatieni Kanuni ambazo zinatokana na sheria zilizotungwa na Bunge letu. Kwa hiyo, Mwanasheria Mkuu lazima asimamie hayo na ameapa kuitetea Katiba, ndiyo maana ya kiapo hicho, kwa maana nyingine aweze kuyasema hata yale ambayo viongozi wa Serikali, hawapendi kuyasikia. Yeye kazi yake ni kushauri tu. Utekelezaji na jinsi gani wanatumia ushauri huo hilo ni suala tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sura hiyo hiyo ya kisiasa unaiona hata kwa Katiba ilivyoandikwa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali hana *tenure* kwamba imekuwa *entrenched* kwenye Katiba, kwa sababu ni mshauri wa karibu sana na Rais, Rais lazima aweze kumwamini huyu kwamba ananipatia ushauri wa kweli na sahihi, isipokuwa kama atajiuzuru yeye mwenyewe hataondolewa mapema anaondoka katika wadhifa huu mara tu Rais mpya anapoapishwa. Hii sura ndiyo mnaiona katika nchi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais Bill Clinton alikuja na *Attonery General* wa kwanza yule mama Janeth, hakutaka kuendelea katika awamu ya pili ya uongozi wake, akaja mwingine kamaliza naye. George Bush akaja na wa kwake Ashcroft lakini naye angeweza kuendelea lakini kwa sababu zingine ameamua kutoendelea. Vile vile Uingereza wakichukua *Labour party* wanaleta *Attonery General* wao, wakichukua *Conservative* wataweka *Attonery General* wao, kwa hiyo, ile hoja ya matani ya rafiki

yangu wa upande wa *CUF* nisiwe na wasiwasi kwamba wao wakikamata eti mimi nitakuwa *Attonery General,* nakueleza mambo hayaendi hivyo. Mwanasheria Mkuu lazima ajue mipaka ya kazi yake. *(Makofi/Kicheko)*

Katika sura hii ya kisiasa wewe lazima uwe mtu unayewezesha siyo kukwamisha maana wanatekeleza sera ambazo wamezinadi kwa wananchi kwamba tukichaguliwa sisi haya tutayafanya na kama yanahitaji kutungiwa sheria yatungiwe sheria. Kama ni kurekebisha sheria yarekebishe sheria na ndiyo maana tuko humu Bungeni na Serikali kuisaidia twendeni tuyafanikishe hayo mliyowaahidi wananchi. Kwa maana hiyo, hawezi akaingia tu humu kama wanavyoingia watumishi wa Bunge, huyu lazima awe na nafasi yake maalum, yeye siyo mshauri wa Bunge, ni mshauri wa Serikali, lakini kwa nafasi yake hiyo akishatoa ushauri ni vizuri hata kama amekalia kiti kingine ambacho huchukii ushauri wake lakini angalau ukisikiliza wamesema nini. Nadhani nimeona niyasema hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama utakavyoona katika orodha ya marekebisho ya ziada eneo la chombo kama Bunge na Mahakama pale ambapo itaonekana kwamba kuna sababu ya msingi kama ilivyoonekana huko nyuma Spika anaburuzwa kwenda Mahakamani. Mwanasheria Mkuu, lazima asimame kwenda kulinda maslahi ya Bunge kwa sababu Bunge ni sehemu moja ya dola ya nchi hii na Mahakama za Tanzania zimetamka kwa hilo kwamba Mwanasheria Mkuu, pale anapoona inafaa kwenda kusimamia kesi inayohusu Bunge au inayohusu Mahakama ana haki ya kufanya hivyo.

Kwa hiyo, hilo nataka niwaondolee wasiwasi kabisa Waheshimiwa Wabunge, kwenye eneo hilo kwamba halina matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilitolewa hoja kwenye Kamati kwamba hii Itifaki iliyopo katika Ibara ya 5(3) Kamati, walisema sawa kwa Mwanasheria Mkuu, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Mashtaka, wanapokwenda Mahakamani tumeelewa ule utambulisho wa kwanza kwamba kama iko kesi inamhusu Mwanasheria Mkuu na aliyekuja ni yeye mwenyewe au Naibu wake au Mkurugenzi wa Mashtaka kwamba wao ndiyo wasikilizwe kwanza, wapewe fursa ya kwanza. Lakini wanapokuja maofisa wengine chini ya hao kwa nini maana wapo Mawakili wakongwe, wengine wamewahi kuwa Wanasheria Wakuu wa nchi hii huko nyuma, wengine ni Mawakili maarufu, wana utumishi wa miaka mingi anakuja tu kijana mdogo tu ana miaka miwili au mitatu tu.

Sasa napenda nijibu hoja hii kwa kusema kwamba naweza nikasema tu kwamba Serikali ndicho chombo pekee chenye umri mkongwe hapa nchini na duniani kote. Utambulisho ambao Mwanasheria Mkuu anapewa, anapewa kwa niaba ya Serikali kwa niaba ya dola. Itifaki hiyo lazima ionekane katika kesi zote ambazo zinaihusu Serikali. Kwa maana hiyo, huwezi ukasema tu kwa sababu aliyefika mbele ya Mahakama au anashikia kesi hiyo kwa niaba ya *Attonery General* ana miaka miwili na hana uzoefu kushinda mimi au kuliko mimi kwamba mimi ndiyo nitangulie, hapana, utakuwa unabomoa msingi. Yule yuko pale kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu, yuko pale kwa

niaba ya Serikali. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Bunge lako lielewe pendekezo la Serikali katika Ibara ya 5(3) katika maana hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ilitolewa hoja na Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala kwamba Ibara ya 10 (3) ambayo inasema; "Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka ya Jinai, ndiyo ataiwakilisha Serikali katika rufaa zote Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa." Sasa akasema maana hapa inasema ni yeye tu atafika huko kote kule. Lakini kifungu kidogo cha 2 kinasema anaweza akakasimu majukumu kwa maafisa hao. Sasa alitaka ufafanuzi hapo. Ufafanuzi wangu kwenye eneo hili ni kwamba kifungu hicho cha 3, lazima ukisoma kwa pamoja na kifungu kidogo cha 2 cha ibara ya 10. Maana yake ni kwamba katika hiyo Ibara ndogo ya 3 ambayo ilikuwa inamsumbua Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, inatambua ile nafasi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, kwamba yeye ndiyo atakayeweza kuwasilisha zile rufaa kwa jina lake kama *DPP* kwa niaba ya Serikali, siyo mtu mwingine. Hilo ni jina, yeye atawasilisha hiyo kwa niaba ya Jamhuri.

Sasa kile kifungu cha kidogo cha 2 ndiyo kinaruhusu sasa yawezekana yeye mwenyewe akaenda kusimamia na kuendesha rufaa hiyo katika ngazi ya Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufaa au anaweza akatuma wasaidizi wake ndiyo unaangukia katika Ibara ya 10 (2). Kwa maelezo hayo hakuna mgongano wowote katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, aliligusia alisema kwenye Ibara ya 6, mamlaka ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hasa ilikuwa hailengi kutambua sheria zingine kama ile Sheria ya Mahakimu ya mwaka 1984. Hapa nikubali tunashukuru kwa mchango huo wa Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, katika marekebisho haya ya ziada mtaona katika Ibara ya (c) tumeongeza kifungu cha 33 ambacho kinasemea katika masuala yote ambayo Mwanasheria Mkuu haruhusiwi kufika maana Mawakili mpaka sasa hivi kwa mujibu wa sheria yetu haturuhusiwi kufika kwenye Mahakama za Mwanzo. Ipo hoja inajengwa labda wakati umefika tuliangalie suala hili.

Lakini mapendekezo haya yanasema yawezekana kesi ikaanzishwa kwenye Mahakama ya Mwanzo na imetokea ambapo Mwanasheria Mkuu hata Mawakili wengine hawaruhusiwi kufika huko, lakini Hakimu akaichukua na tunajua hana mamlaka nayo *(Jurisdiction)* sasa hatuwezi tukasema *we are helpless,* hatuwezi kufanya chochote ndiyo maana tunaiandika, tunapendekeza kwa namna hiyo kwamba katika hali hiyo Mwanasheria Mkuu aweze kufika huko na kusema Mheshimiwa Hakimu, hili suala linaondoka kwako lipelekwe mahali ambapo linapaswa liwe ndiyo hayo tunayoyasemea hayo. Tumeisahihisha hiyo ili inyooke vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, aliigusia pia kwamba Ibara ya 8 ya Muswada inayohusu majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, inakinzana kidogo na Ibara ya 11 katika mambo mawili, anasema: *"DPP* mbona anaonekana anaingiliwa ingiliwa na Mwanasheria Mkuu." Dhana ya uhuru Mkurugenzi wa Mashtaka uko katika maeneo matatu tu.

Eneo la kwanza ni hili la kuanzisha mashtaka, eneo la pili, kuyasimamia kwa maana ya kuendesha na tatu hii ya kuweza kuyaondoa. Hayo ndiyo tunasema huwezi

ukamwingilia *DPP* katika hizo *core functions* zake hizo. Lakini nje ya himaya yake hiyo, huyu anafanya kazi chini ya mwavuli wa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Katika maana hiyo, yapo masuala mengi ambayo yanahusu utekelezaji wa Sera za Serikali ambazo na yeye kama sehemu ya Serikali anapaswa azingatie.

Kwa hiyo, kifungu cha 8(1) kinaeleza tu kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ni pana, ndani yake kuna ile Kurugenzi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na ndani yake kuna shughuli zingine, utakuta kama alivyosema Ofisa wangu wa zamani Mheshimiwa Philip Marmo, kuna hii ya uandishi wa sheria na yenyewe imo ni sehemu ya shughuli za Mwanasheria Mkuu. Zipo za Kabidhi Wasii haya masuala ya mirathi, haya masuala ya ndoa, talaka, vifo na masuala ya *bankrupts* yote haya utayakuta ingawa sehemu moja tumenyofoa kumpelekea Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na Mheshimiwa Rita Mlaki.

Lakini hii ndiyo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, ina majukumu mapana, mengine mnayaona ya mikataba haya. Lakini kile kinachosemwa katika Ibara ya 11(1) utekelezaji wa Sera za Serikali kimeandikwa katika njia ya kwamba ukisoma sasa kifungu kidogo cha 11(2) ndiyo kinahifadhi ule uhuru wa *DPP* katika yale maeneo matatu niliyoyasema. Kinasema; *"Nothing in this section shall be construed as abrogating or in anyway limiting the powers of the DPP in relation to the control of public prosecutions."* Kwa maana hiyo, mengine yote mnaweza mkaelekeza, maana ni utekelezaji wa shughuli za Serikali, lakini kwa hayo maeneo yake ya *core functions* hamwezi mkamwingilia.

Kwa hiyo, ukishalielewa hilo na ukikisoma kifungu cha 8(1) kinaanza na maneno; *"Without prejudice to the general provisions of article 59 and 59 (b) of the constitution,"* (bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 59 na 59 (b) ya Katiba). Ukienda kule ndiyo utakuta zile *functions,* kwamba ikifika katika kuamua kuanzisha mashtaka, kuendesha mashtaka, kusimamia na kuondoa hiyo ni ya *DPP* peke yake. Nimeona nilielezee hilo kwa sababu Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, aliliongea kwa nguvu sana. Lakini huwa nawaambia hakuna mtu mwenye *monopoly* ya *knowledge* labda uzoefu tu kidogo mnaweza mkapishana, *knowledge* unaweza ukaipata. Tunamshukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba huu Muswada kama unavyopendekezwa aliuelezea kwa ufasaha sana Mheshimiwa mtoa hoja na ningelipenda sana Bunge lako Tukufu lisimwangalie Mwanasheria Mkuu aliyepo sasa hivi, tuangalie *Institution the Office.* Mwanasheria Mkuu aliyepo anaweza akawa na mapungufu yake kama binadamu yoyote na yeye ni wa kupita. Ofisi hii itaendelea kuwepo na ni vizuri tukiimarisha na ni vizuri Serikali ikaendelea kusimamiwa kwa maana ya kufuata sheria na taratibu na hasa Katiba. Lakini vile vile tukajenga kada ya Mawakili wa Serikali na *Legal Officers* wengine wenye uwezo wa kuisaidia Serikali katika kutoa ushauri wa kisheria ambao ni imara. Ninaposema Serikali nina upana kufika hata kwenye Halmashauri zetu. Lengo hili siyo kuleta *red tape,* urasimu katika shughuli za Serikali lakini ni kuhakikisha kwamba Serikali inapata ushauri sahihi na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani baada ya maelezo hayo nawaombeni sana Waheshimiwa Wabunge, tumuunge mkono Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, ili Muswada huu tuweze kuupitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru wewe na pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru kwa fursa hii ili kufanya majumuisho ya Muswada huu wa *The Attonery General Discharge of Duties Act 2005.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja mbalimbali zimejitokeza wakati wa kujadili Muswada huu. Kabla ya kutoa maelezo kuhusu hoja hizo napenda niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia ambao ni hawa wafuatao, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Semindu Pawa na Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Remidius Kissassi na Mheshimiwa *Lady* Asha Ngede. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kukubaliana na dhana ya malengo ya Muswada huu. Napenda niyatolee maelezo maeneo mbalimbali ambayo Waheshimiwa Wabunge, ama wamehitaji ufafanuzi au wameshauri yafanyiwe marekebisho katika Muswada huu. Imetolewa hoja kwamba utaratibu unaopendekezwa utaleta mgongano kati ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mamlaka zinazoajiri wanasheria wengine pale Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakapochukua hatua dhidi ya mwanasheria aliyekiuka maadili.

Naomba kuwatoa hofu Waheshimiwa Wabunge, kuhusu utaratibu unaopendekezwa na Serikali. Mamlaka ya nidhamu kwa wanasheria ambao hawapo moja kwa moja chini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itakuwa ni waajiri wao. Mwanasheria Mkuu atakuwa na mamlaka ya nidhamu kwa Mawakili wa Serikali tu kwa maana nyingine *State Attorneys.* Lakini endapo wanasheria wengine waliopewa wadhifa wa Uwakili wa Serikali na Mwanasheria Mkuu wa Serikali watakiuka maadili ya kazi. Inapendekezwa kwamba Mwanasheria Mkuu awe na uwezo wa kuwaondolea wadhifa huo. Hivyo masuala mengine ya nidhamu yataendelea kuwa chini ya mwajiri wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetolewa hoja kwamba kutokana na kuitambua Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Kikatiba itenganishwe na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kiutendaji. Majukumu ya msingi yanayompa Mkurugenzi wa Mashtaka uhuru wa kutoingiliwa na mamlaka nyingine kama nilivyosema katika mjadala wa mabadiliko ya 14 ya Katiba ni kufungua, kuendesha au kuondoa mashtaka tu na kama alivyofafanua hivi punde Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Usimamizi wa ajira za watumishi waliopo chini yake utaendelea kuwa chini ya utaratibu wa kawaida wa ajira ya watumishi wa Serikali.

Kuhusu mapendekezo ya jina la Mkurugenzi wa Mashtaka kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai, Serikali inaona kwamba liendelee kubaki kama lilivyo hivi sasa.

Mifano iliyotolewa kwamba kuna mashtaka ya ndoa, madai na kadhalika, si sahihi kwa kuwa ni neno linaloashiria vitendo vya jinai. Masuala mengine ni ya madai au malalamiko tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetolewa hoja kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali asiwe mwanasiasa. Kama nilivyoeleza wakati nahitimisha Muswada wa mabadiliko ya Katiba Mwanasheria Mkuu wa Serikali ana sura mbili ya kiutekelezaji na kama Mbunge kama alivyofafanua mwenyewe hivi punde.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetolewa hoja ya kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, akishateuliwa na Rais athibitishwe na Bunge na uwajibikaji wake uwe kwa Bunge. Muundo wetu wa uongozi ni wa Kirais. Serikali kwa ujumla wake ndiyo ina wajibika Bungeni na si uwajibikaji wa mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja imetolewa kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali asipewe majukumu ya kushughulikia Mikataba kwa mujibu wa Sheria ya *Public Procurement Act* kwa sababu hawajibiki Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 59(3) ya Katiba ya nchi inamtaka kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiye mshauri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya mambo ya sheria. Hivyo ana wajibu wa Kikatiba wa kushauri. Kama nilivyokwisha kueleza mfumo wetu wa uongozi ni wa Kirais hivyo inapendekezwa Mwanasheria Mkuu aendelee kuwajibika kwa mamlaka ya uteuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, imependekezwa kwamba Mkurugenzi wa Mashtaka asiwe chini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pamoja na Mkurugenzi wa Mashtaka kuwa ofisi nzito na yenye majukumu mazito. Uhuru uliopo kwake ni wa kufungua, kuendesha na kuondoa mashtaka tu, masuala mengine hususan ya kisera yataendelea kusimamiwa na mamlaka nyingine ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetolewa hoja kwamba maneno maslahi ya umma yaondolewe katika Ibara ya 14 kwa vile yanaweza kutumiwa vibaya na Serikali. Napenda kuwaondoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kuhusu suala hili. Ni kweli kwamba Mahakama hutoa tafsiri juu ya maneno maslahi ya umma. Hata hivyo, ili Mahakama iweze kupima iwapo hatua ya Serikali ilikuwa kwa maslahi ya umma au laa. Sheria lazima iweke kigezo hicho. Serikali inaona kwamba msingi huu lazima uwepo katika Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetolewa tahadhari kuwa utaratibu tunaouanzisha wa mawasilino na Mwanasheria Mkuu wa Serikali usisababishe *red-tape* katika utendaji kazi. Nakubaliana na tahadhari hiyo. Hata hivyo, hatutegemei hilo kujitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumzwa suala la kucheleweshwa upelelezi katika mashauri ya jinai. Kimsingi mwenye mamlaka ya upelelezi ni Polisi kwa kupitia Ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Jinai. Hata hivyo, kama Serikali, tumeipokea hoja hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine inahusu kufanya marekebisho katika Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai ili kuzingatia maudhui ya Muswada huu. Mapendekezo hayo yatashughulikiwa katika Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali utakaowasilishwa baadaye wakati wa Mkutano huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetolewa hoja kwamba hoja itaje wakati gani Mwanasheria Mkuu wa Serikali ataingilia shughuli za Mkurugenzi wa Mashtaka, Mwandishi Mkuu wa Sheria na Kabidhi Wasii Mkuu. Kuhusu Mkurugenzi wa Mashtaka, Ibara ya 11(1) ya Muswada inamwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kusimamia masuala ya kisera.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetolewa hoja pia kwamba majukumu ya kuendesha mashtaka yawe kwa Mkurugenzi wa Mashtaka pekee, polisi wafanye kazi ya upelelezi. Kimsingi mamlaka ya uendeshaji mashtaka yapo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka. Kutokana na kutokuwepo Mawakili wa Serikali wa kutosha, Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai imempa *DPP* mamlaka ya kuwateua Maofisa wengine kutekeleza baadhi ya shughuli zake, miongoni mwa Maofisa hao ni polisi. Hata hivyo, ili kuimarisha jukumu la uendeshaji wa mashtaka, Serikali inao mkakati wa kuondoa majukumu hayo kutoka kwa vyombo vingine vilivyopewa mamlaka ya kuendesha mashtaka. Mkakati huu unalenga kusambaza shughuli za Mkurugenzi wa Mashtaka hadi Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyotolewa ilitaka maelezo juu ya namna ambayo Kabidhi Wasii Mkuu anavyodhibitiwa hususan anayehodhi ruzuku ya chama cha siasa. Kabidhi Wasii Mkuu hana uhusiano kabisa na masuala ya ruzuku na vyama vya siasa. Hata hivyo, mwongozo wa namna anavyodhibitiwa upo katika Sheria mbalimbali zinazoshughulikia majukumu yake. Vile vile kwa Wizara anawajibika moja kwa moja kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetolewa tahadhari kuhusu kumpa mamlaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya kusimamia mfumo mzima wa kutoa ushauri wa Serikali na vyombo vyake na kwamba ni kinyume na dhana nzima ya kupeleka madaraka ngazi za chini hususan Mamlaka ya Miji na Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo unaopendekezwa kwenye Muswada huu haulengi katika kuhodhi mamlaka ya utoaji ushauri bali lengo lake ni kuboresha mfumo huo. Mamlaka ya moja kwa moja ya usimamizi atakayokuwa nayo Mwanasheria Mkuu wa Serikali yatawahusu Mawakili wa Serikali tu. Wanasheria wengine watasimamiwa na waajiri wao wanapotekeleza majukumu yanayohusu Wizara, Idara na Taasisi za Sheria. Maeneo yanayotengwa kwa ajili ya Mwanasheria Mkuu hawatapaswa kuyatekeleza. Kwa mfumo huu Mwanasheria Mkuu hataingilia uhuru wa mamlaka za Miji wala Halmshauri za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetolewa hoja kwamba kwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiye atawateua watu kuwa Mawakili wa Serikali hata wale walio

katika Wizara, Idara na Taasisi nyingine za Serikali chini ya kifungu cha 24(3) cha Muswada, basi kwa kufanya hivyo watawajibika kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusisitiza kwamba uwajibikaji huu utahusisha utekelezaji wa majukumu kwa Mawakili wa Serikali wanaowajibika moja kwa moja kwa Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, kwa mara nyingine tena napenda nikushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria inayoainisha Majukumu na Kazi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2005 *(The Attorney General (Discharge of Duties) Bill, 2005***

Jina la Muswada

*(Jina la Muswada lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 4
Kifungu cha 5

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 6

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 7

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 8
Kifungu cha 9

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 10

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 11
Kifungu cha 12
Kifungu cha 13

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 14

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 18
Kifungu cha 19

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 25
Kifungu cha 26

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 27

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 28
Kifungu cha 29

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 30

Kifungu cha 31

Kifungu cha 32

Kifungu cha 33

*(Kifungu kipya kiliyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria inayoainisha Majukumu na Kazi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2005 *(The Attorney General (Discharge of Duties) Bill, 2005***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge Zima imeufikiria Muswada huu na kuukubali pamoja na mabadiliko yaliyofanywa. Hivyo natoa hoja kwamba Muswada wa *The Attorney General (Discharge of Duties) Act, 2005* kama ulivyobadilishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

*(Saa 11.45 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi Tarehe 10 Februari, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*